





**Waziri** Aweso atumbua tena vigogo wa maji

UKURASA 3




UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Januari 8, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581184

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


RIPOTI MAALUM

# Simulizi ya kijana aliyekaa mahabusu polisi kwa siku 89

• **Wanasheria** watoa mbinu kumaliza tatizo... *Ukurasa. 4*



## Mwalimu mwenye ulemavu wa macho abuni mtambo wa kuzalisha umeme

UKURASA 5



# Rais Samia asikia kilio cha ucheleweshaji kesi

UKURASA 2

MICHEZO SAA ZAHESABIKA HATIMA FEI TOTO UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Rais asikia kilio ucheleweshaji kesi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameteua wajumbe 11 wa Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai nchini inayoongozwa na Mwenyekiti, Jaji Mohamed Chande na Makamu Mwenyekiti, Katibu Mkuu Kiongozi mstaafu, Balozi Ombeni Sefue.

Taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa juzi usiku na Zuhura Yunus, Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, ilibainisha wajumbe wengine wa tume hiyo ni: Jaji Dk. Eliezer Feleshi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG); Dk. Laurean Ndumbaro, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Utumishi; Said Mwema, Mkuu wa Jeshi la Polisi mstaafu; na Balozi Ernest Mangu, Mkuu wa Jeshi la Polisi mstaafu.

Pia wamo Dk. Edward Hoseah, Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS); Saada Makungu, askari polisi mstaafu; Omar Issa, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Umeme (TANESCO); Baraka Leonard, ofisa mwandamizi, Ofisi ya Rais; na Yahya Khamis Hamad, Mkurugenzi wa Utafiti katika Chuo Kikuu cha Zanzibar na Rais mstaafu wa Chama cha Wanasheria Zanzibar.

### JICHO LA CAG

Wakati Rais Samia akiteua wajumbe hao wa tume hiyo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ameripoti kuwa kuna shida katika kutoa haki kwa haraka na kwa usawa kwa mamlaka zinazohusika na haki jinai nchini.

Katika ripoti yake ya ukaguzi maalum wa utoaji wa haki jinai nchini iliyowasilishwa bungeni Aprili 12 mwaka jana, CAG Charles Kichere anasema mahakama inatakiwa kutoa haki kwa wote bila kuchelewa na bila kujali hadhi ya mtu pamoja na kuzingatia weledi.

Anafafanua kuwa ucheleweshaji wa haki unatafsiriwa kama muda unaotumika kumaliza

kesi unaozidi muda wa kawaida uliowekwa, unaotarajiwa kutumika kuamua kesi mahakamani.

"Imethibitika kuwa ucheleweshaji wa kesi hukwamisha na kuchelewesha shughuli za kiuchumi na kimaendeleo za mtu binafsi. Kwa hiyo, haki ikicheleweshwa, migogoro hubaki bila kutatuliwa na hivyo watu hawataweza kupata usalama na hifadhi kwa wakati," anahadharisha.

CAG anabainisha kuwa kutokana na idadi ndogo ya waendesha mashtaka nchini, pamoja na wajibu wa uchunguzi, Jeshi la Polisi linafanya kazi ya kusimamia mashtaka ya watuhumiwa wanapofikishwa mahakamani.

Anaendelea kufafanua kuwa ingawa kumekuwa na mipango ya kuhakikisha jukumu la uendeshaji wa mashtaka wanaachiwa mawakili wa serikali, kutokana na idadi ndogo ya mawakili, zipo mahakama ambazo mashtaka yamekuwa yakiendeshwa na maofisa wa polisi.

Katika ripoti yake hiyo, CAG pia anabainisha kuwa jumla ya Sh. bilioni 8.509 zilipatikana kutoka Benki ya Dunia kama moja ya hatua za kupunguza mrundikano wa mashauri katika mfumo wa mahakama.

Anasema mahakama iliunda Mfumo wa Usimamizi wa Kesi Kielekitroniki ili kuongeza ufanisi katika mifumo ya kimahakama ya utoaji haki.

Anasema maofisa wa mahakama hutumia mfumo huo katika usajili wa kesi, usimamizi na uandaaji wa takwimu. Pia hitaji la kumbukumbu zote rasmi za mahakama kuwasilishwa katika jalada la kesi la kielekitroniki limefanywa kuwa la lazima.

Zaidi ya hayo, CAG anasema Mahakama ya Tanzania pia iliunda malengo ambayo yaliweka kiwango cha chini cha idadi ya mashauri yanayopaswa kumalizwa kwa muda maalum kwa majaji na mahakimu.

Kwa majaji wa Mahakama Kuu, kesi 220 zilipaswa kumalizika ndani ya miezi 24; kwa mahakimu wa mahakama za hakimu mkazi na mahakama za wilaya, kesi 250 zilipaswa kumalizika ndani ya miezi 12.

Katika ukaguzi wake uliohusisha kipindi cha miaka sita ya fedha 2015/16 hadi 2020/21, CAG anasema Mahakama Kuu haikufikia kiwango cha asilimia 100 cha kumaliza kesi kwa sababu kesi zilizofunguliwa kwayo hazikumalizika ndani ya muda uliopangwa.

"Kesi za jinai ambazo hazijatatuliwa zimekuwa zikisogezwa mbele na hivyo kuongeza ucheleweshaji na mrundikano wa kesi mahakamani.

"Kulikuwa na kesi ambazo zilichukua zaidi ya miaka saba kukamilika. Kuwapo kwa kesi za jinai ambazo zimekaa zaidi ya muda uliowekwa kunaitaka mahakama kuweka utaratibu wa kuzishughulikia kupitia mfumo ili kupunguza mrundikano wa kesi.

"Matokeo ya ukaguzi pia yalionyesha kuwa kulikuwa na wastani wa hakimu mmoja kwa kila mahakama na majaji wawili kwa Mahakama Kuu ambao walifanikiwa kufikia lengo lililowekwa la kumaliza kesi 250 kwa mahakimu na kesi 220 kwa majaji.

"Ni mahakimu watatu tu waliweza kufikia zaidi ya kesi 100 katika mahakama za hakimu mkazi zilizotembelewa," CAG anabainisha na kuvitaja vikwazo kwamba vinajumuisha Mahakama Kuu kutokusimamia ipasavyo vikao vya kesi za jinai; Mahakama haikushirikisha ipasavyo wadau wakuu katika kupanga mikakati ya kupunguza na kumaliza kesi za jinai; na ugawanaji usio sawa wa kesi (mzigo wa kazi) baina ya mahakimu.



Rais Samia Suluhu Hassan.

CAG pia anasema kuwa kutokana na mahojiano yaliyofanywa kati ya timu ya ukaguzi na

viongozi wa Mahakama ya Tanzania na mapitio ya mashauri, ilibainika kesi za jinai Mahakama Kuu zilichukua hadi miaka minne kabla ya kuitishwa kwa kikao cha kwanza na hakuna kesi iliyoisha ndani ya kikao kimoja.

Pia, ilibainika hapakuwa na uhakika wa kesi kupangwa kusikilizwa katika vikao mfululizo, jambo ambalo liliongeza ucheleweshaji wa utoaji wa haki.

"Muda wa chini uliotumika hadi kukamilika kwa kesi za jinai ulikuwa miezi 32.7 kwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya. Hali hii imesababisha kuongezeka kwa kesi katika mahakama za chini na washtakiwa kukaa mahabusu muda mrefu bila kusikilizwa.

"Zaidi ya hayo, ilibainika kuwa kesi hizi ziliongeza mzigo kwa mahakimu wakazi na hivyo kuathiri uwezo wa kumaliza kesi zao walizopangiwa," anabainisha.

### UHABA WA WATUMISHI

CAG anasema Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikal ina waendesha mashtaka 661 badala ya 5,890 sawa na upungufu wa asilimia 89 na kwamba ingawa Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali haijaweka idadi ya kesi zinazoweza kuendeshwa kwa mwaka na mwendesha mashtaka mmoja, kumeonekana kuwa idadi kubwa ya kesi zilikuwa zikisimamiwa na mwendesha mashtaka mmoja kwenye baadhi ya Mahakama Kuu na mahakama za hakimu mkazi.

"Kwa mfano, katika Mahakama Kuu ya Mbeya, mwendesha mashtaka mmoja alitakiwa kushughulikia wastani wa kesi za jinai 289 kwa mwaka; wakati katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha, mwendesha mashtaka mmoja alitakiwa kushughulikia kesi za jinai zipatazo 325 kwa mwaka.

"Wastani huu unaonyesha kuwa upande wa mashtaka una mzigo mkubwa wa kazi. Jitihada za kupunguza mchakato na muda unaotumika kufanya upelelezi na kupunguza tatizo la ucheleweshaji wa utoaji wa haki unahitaji kuimarishwa," anashauri.

### HAKUNA MAFUNZO

CAG pia anasema ukaguzi wake pia umebaini kuwa kuanzia mwaka 2018 hadi 2021, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali haikufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo.

"Hakukuwa na kanzidata au kumbukumbu inayoonyesha upungufu wa ujuzi kwenye Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali ambayo ingesaidia kupanga bajeti na kuweka vipaumbele vya mafunzo katika kila mwaka wa fedha.

"Maofisa wa Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali walionyesha kuwa katika siku za nyuma mafunzo yaliendeshwa bila mpangilio, na badala yake mafunzo yaliendeshwa kwa kuzingatia mahitaji au maelekezo ya wafadhili juu ya nini kinapaswa kuwasilishwa katika programu za mafunzo. "Uchambuzi wa sababu za changamoto hizo ulibaini kuwa tathmini ya mahitaji ya mafunzo haukupewa kipaumbele na Idara ya Usimamizi wa Kesi. Idara hii ilijikita zaidi kwenye kazi zingine kama za kitaalamu na kiutawala.

"Matokeo yake, imekuwa vigumu kutathmini uwezo na mahitaji halisi ya mafunzo kwa wafanyakazi. Hata hivyo, baada ya uchunguzi zaidi kuhusu kuwajengea uwezo waendesha mashtaka, ilibainika kuwa idadi ndogo ya waendesha mashtaka na mzigo mkubwa wa uendeshaji wa kesi ilikuwa sababu mojawapo ya waendesha mashtaka kutopelekwa mafunzoni," anafafanua.

### MUDA WA UPELELEZI

Kwa mujibu wa Sheria ya Polisi Wasaidizi (Kanuni za Kudumu za Polisi) ya mwaka 2021, upelelezi wa makosa ya jinai unapaswa kukamilika ndani ya mwaka mmoja kwa makosa makubwa na miezi sita kwa makosa mengine.

Hata hivyo, CAG anasema kuwa maofisa wa upelelezi wa makosa ya jinai waliohojiwa, walieleza kuwa muda wa upelelezi uliowekwa haukuwa na uhalisia na utekelezaji wake ulikuwa mgumu na mara chache ulifikiwa.

"Ukaguzi ulibaini Jeshi la Polisi lilitumia vyombo vingine kama Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, kampuni za mitandao ya simu, Mamlaka ya Mapato Tanzania na taasisi za fedha (benki) katika kusaidia uchunguzi na upelelezi wa kesi.

"Ushirikishaji huu umeonekana kuchukua muda mrefu. Mathalani, Mkoa wa Mbeya ilionekana kuwa na uchelewaji mkubwa ambapo kwa sampuli zilizopelekwa kwa Mkemia Mkuu wa Serikali zilichukua zaidi ya siku 366 bila majibu kupelekwa Jeshi la Polisi kwa hatua zaidi. Hali hii ilisababishwa na ukweli kuwa upimaji wa sampuli hufanyika katika maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali pekee iliyoko Dar es Salaam. "Pia ilibainika kuwa hapakuwa na idadi ya kutosha ya maofisa wa upelelezi ndani ya Jeshi la Polisi, hivyo kuwa miongoni mwa sababu zilizochangia kuchelewa kwa shughuli za upelelezi," CAG anafafanua.

### HOJA YA CAG

Kwa ujumla, CAG anasema ukaguzi wake umebaini kuwapo upungufu katika mfumo wa haki-jinai unaosababisha ucheleweshaji wa utoaji wa haki na kwamba hali hiyo ina athari za kijamii na kiuchumi kwa mtu binafsi na taifa kwa ujumla.

Anasema ucheleweshaji wa utoaji wa haki kwa kuzingatia uchelewaji wa kusikiliza kesi ni kinyume cha Lengo Na. 16 la Malengo ya Maendeleo Endelevu. "Wadau wote wakuu katika mfumo wa utoaji wa haki nchini wahakikishe wanaongeza juhudi za kutatua changamoto hii ya

usheleweshaji wa kesi. Hali hii inaashiria kwamba sababu za msingi za upungufu uliobainika hazijashughulikiwa ipasavyo.

"Pia, ukaguzi huu umeonyesha kwa kiasi kikubwa utoaji wa haki nchini hauratibiwi ipasavyo; wadau wakuu kwenye mfumo wa utoaji wa haki wakiwamo Mahakama ya Tanzania, Jeshi la Polisi na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali hawajawekeza ipasavyo kwenye kutatua tatizo la ucheleweshaji wa kesi pamoja na kukosekana kwa dhamira ya pamoja katika kuhakikisha kuwa udhibiti wa ucheleweshaji wa kesi katika mfumo wa utoaji wa haki unaimarishwa," CAG anawasilisha hoja yake.

Pengine wajumbe 11 wa tume iliyoteuliwa na Rais wataifanyia kazi hoja hii ya CAG.



Shekhe Santokh Singh (wa pili kulia), akikabidhi kwa Mmiliki wa Kituo cha Yatima Group Trust Fund,Winfrida Alfred, vyakula na vifaa mbalimbali vya wanafunzi wanaolelewa katika kituo hicho, vilivyotolewa na Taasisi ya Singa Singa, Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Aweso atumbua vigogo wengine

**Na Christina Haule,** MLIMBA

MENEJA wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) mkoani Morogoro, John Msengi na Meneja wa Wilaya ya Kilombero, Florence Mlelwa wamelazimika kurudishwa wizarani kupangiwa majukumu mengine baada ya kushindwa kutekeleza na kusimamia utekelezaji wa miradi ya maji kwenye Tarafa ya Mlimba wilayani Kilombero.

Akiwa kwenye ziara yake ya siku tisa kukagua na kuzindua miradi ya maji mkoani hapa jana, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso alisema pamoja na mafanikio aliyoyaona katika utekelezaji wa miradi ya maji kwenye baadhi ya miradi aliyotembelea, kuna maeneo mengine hayajapatiwa ufumbuzi kutokana na kukwamishwa na watu wachache licha ya serikali kutoa fedha.

Waziri Aweso alisema amelazimika kuwasimamisha kazi kwenye vituo vyao baada ya kutoridhishwa na majibu ya mameneja hao kuhusu ujenzi na utekelezaji wa Mradi wa Maji Kalengakero wenye thamani ya Sh. milioni 282 na Mradi wa Maji Mlimba wenye thamani ya Sh. milioni 600.

Mbali na kuwarudisha wizarani viongozi hao, Waziri Aweso pia amevunja Bodi ya Maji Mlimba na kuagiza kuundwa kwa Mamlaka ya Maji Mlimba ambayo itakuwa na uwezo ya kuwahudumia wananchi wa eneo hilo na kutatua kero zao za maji.

"Haiwezekani mimi nitoke wizarani nije kutatua changamoto za maji za watu wa Morogoro wakati mamlaka husika zipo, lazima kila mtu awajibike kwa nafasi yake na kama hawezi hana budi kutupisha," alionya.

Akiwa njiani, Waziri Aweso alisema alisimamishwa na wananchi wa Kijiji cha Kalengakero wakiwa na mabango yenye ujumbe mbalimbali za malalamiko ya kukosa maji licha ya kuwa na chanzo cha maji kinacholisha Mji wa Mlimba na vitongoji vyake.

"Hawa wataalamu wetu baada ya kusikia tunakuja, kuna kijiji hapo kinaitwa Kalengakero wananchi walinisimamisha wakawa wanalalamika kwamba 'hatupati maji na leo kama yametoka ni kwa sababu wamejua wewe unakuja'.

"Juu kwenye tangi nikawaambia hili tangi tumeliona, nipitisheni kwenye vituo vitano ambavyo vinatoa maji, yeye mwenyewe havijui, wakanibabaisha, mwananchi mmoja akanipeleka kwenye kituo kimoja pale, ninafungua maji yakatoka nikamwambia ninaomba tufuatishe hili bomba, kumbe wameunganisha mpira kinyume ili pale maji yatoke na nikiondoka maji yakatike na baadaye wasema waziri kaondoka na maji yake," alisema.

Waziri Aweso alishangazwa na Meneja wa RUWASA Wilaya ya Kilombero kushindwa kutumia Sh. milioni 600 ambazo serikali imezitoa miezi kadhaa iliyopita kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji wilayani humo ili kuondoa kero ya maji kwa wananchi.

"Ni kweli kama fedha hizo zingetumika ilivyokusudiwa sasa hivi mama zangu na dada zangu msingekuwa mkipiga kelele, bali mngeutumia muda wenu vizuri, badala ya kutoka usiku kutafuta maji, mkiwaacha baba zangu wamelala na baridi kali," alisema Aweso.

Waziri huyo alisema Mlimba siyo masikini wa vyanzo vya maji, akibainisha kuwa amepita kwenye madaraja na kushuhudia maji yakitiririka.

Mmoja wa wananchi wa Kijiji cha Kalengakero, Sara Rashidi alimwomba waziri kuwatatulia kero ya maji kijijini huko kwa kuwa pamoja na kuwa na chanzo cha maji kijijini, maji hayo yanachukuliwa na kupelekwa mjini Mlimba na kuwaacha wenyeji wakikosa huduma hiyo.

Mbunge wa Mlimba, Godwin Kunambi alisema hali ya upatikanaji wa maji jimboni huko hairidhishi licha ya serikali kupeleka fedha nyingi za miradi ya maji.

Kunambi aliishukuru wizara kwa kusaidia jimbo lake kupata miradi ya maji ukiwamo wa Mbingu Igima ambao unasambaza maji kwenye vijiji vinne kati ya sita vilivyopo, akimwomba waziri kuangalia namna ya kusaidia vijiji vyote kupata maji.

Mbunge huyo alieleza kusikitishwa na Meneja wa RUWASA Wilaya kwa kushindwa kutekeleza mradi wa maji katika Tarafa ya Mlimba ili wananchi wapate maji ya uhakika licha ya serikali kutoa Sh. 600 kwa ajili ya mradi huo.

Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Hanji Godigodi aliiomba Wizara ya Maji kutoa mwongozo wa ankara za maji ambao utaonyesha gharama halisi za maji ili kuondoa malalamiko ya wananchi kuhusiana na kuzidishiwa malipo ya huduma hiyo.

Kiongozi huyo pia alisisitiza wananchi kutunza vyanzo vya maji na miundombinu iliyopo ili kutumika kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

## Viwavijeshi wavamia mashamba

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WILAYA tatu za Mkoa wa Singida zimevamiwa na viwavijeshi ambao wameanza kuharibu mimea mashambani na kuzua hofu kwa wakulima.

Wilaya zilizovamiwa na wadudu hao hatari kwa uharibifu wa mazao ni Mkalama, Iramba na Singida Vijijini.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba alisema jana kuwa kutokana na hali hiyo Wizara ya Kilimo imejulishwa na maofisa wake wameshafika kwenye wilaya hizo kufanya tathmini.

Serukamba aliwaagiza maofisa ugani wa kata wakati serikali inaendelea kufanya tathmini waelimishe wakulima wanunue dawa za kuulia wadudu hao.

"Tumevamiwa na viwavijeshi lakini mabwana kilimo mjitahidi mkanunue dawa tukapulizie hao wadudu wanaweza kuondoka, tumeshatoa taarifa Wizara ya Kilimo na timu ya maofisa wa wizara ipo wilayani Itamba na Mkalama kufanya tathmini," alisema.

Mkuu wa Mkoa huyo pia aliwataka maofisa kilimo kuwafikia wakulima kuwaelewesha njia za kilimo cha kisasa kitakachoendana na mabadiliko ya hali ya hewa na kuwasaidia namna bora ya kukabiliana na viwavijeshi.

Alitoa agizo hilo wakati akikagua vituo vya kufanyia majaribio ya mbegu za mazao ya kimkakati katika Halmashauri ya Wilaya za Singida na Ikungi.

Serukamba alisema serikali imeamua kuanzisha 'Viwavi Source Center' kuangalia aina gani ya mbolea itafaa katika mazao ya aina fulani ili matokeo yake yakiwa mazuri, yatakuwa msaada kwa wakulima maeneo ya vijijini.

"Lengo la kuanzisha hivi Viwavi Source Center ni kukabiliana na changamoto zinazowakumba wakulima na tumegawanya maeneo vipande vipande ili kuona mbolea gani itatumika kwenye mazao fulani ambapo matokeo yake ndiyo yataanza kutumiwa na wakulima," alisema.

Serukamba aliongeza kuwa wataalamu wa kilimo wasijifungie ofisini wakawatelekeza wakulima pekee yao kipindi hiki cha uzalishaji, hivyo waendelee kufika mashambani kuwasaidia utaalamu wa kilimo chenye tija hasa matumizi ya mbolea, dawa na namna ya kupalilia.

Kuhusu suala la wakulima kulima zao moja, Serukamba aliwataka maofisa kilimo kuwaelimisha wakulima hao kugawa mashamba ili walime mazao tofauti tofauti kuliko kuamini moja ambalo hali ya hewa ikibadilika mavuno yanakuwa chini.

Diwani wa Mudida, Omary Mande alimweleza Mkuu wa Mkoa kuwa changamoto inayosababisha wakulima wengi katika halmshauri hiyo kushindwa kutumia mbolea ni umbali wa kuifuata mbolea hiyo, hivyo akaomba wakulima wasogezewe huduma hiyo.

Mande alisema kuwa wakulima wengi wa Halmashauri ya Singida wako mbali na vituo inakopatikana



# Simulizi ya kijana aliyekaa mahabusu ya polisi siku 89

Na Halfani Chusi

HAKI ya kupewa dhamana kwa mtuhumiwa ni ya kisheria na kwa namna yoyote ile mtuhumiwa anapokuwa mikononi mwa polisi, hapaswi kunyimwa haki hiyo, mradi tu ametimiza vigezo vya kuipata.

Kwa makosa ambayo hayadhaminiki, mtuhumiwa anatakiwa kufikishwa mahakamani ndani ya saa 24 tangu alipokamatwa, isipokuwa kwa makosa yanayohusiana na adhabu ya kifo, kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai inayotumika nchini kwa sasa.

Huku kukiwa na angalizo hilo la kisheria, Nipashe imebaini baadhi ya askari wa Jeshi la Polisi wasio waadilifu, wamekuwa wakiwanyima dhamana baadhi ya watuhumiwa wenye haki ya kuipata, ikiwa ni njia mojawapo ya kutengeneza mianya ya kujipatia fedha (rushwa).

Ushuhuda wa kijana Bahati Mbugi (29) aliyekaa mahabusu ya polisi kwa siku 89 (miezi mitatu) unabeba tafsiri ya majibu ya maswali kuhusu madhila yanayowakumba watuhumiwa wanaowekwa kwenye mahabusu za jeshi hilo.

Ni ukakasi katika utendaji wa Jeshi la Polisi ambao Agosti mwaka jana ulinyooshewa kidole kilichoambatana na karipio kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassan, aliyemwelekeza Mkuu wa Upelelezi Makosa ya Jinai (DCI) kuchukua hatua kuudhibiti.

"Nimepokea taarifa ya hatua mlizozichukua katika jitihada za kuharakisha upelelezi ili kupunguza mrundikano wa mahabusu kwenye vituo vya polisi na magerezani, kuhakikisha kuwa ile tabia ya kuwabambikizia wananchi kesi inakoma.

"Na mimi ninaliunga mkono hilo na ninawataka mlifanye kwa haraka sana, nimepewa taarifa hapa kwamba kesi 1,840 zimefutwa. Hazikuwa na ushahidi wa maana, polisi tu kwa kutumia nguvu yake na crown yake 'kamata twende peleka' na pengine ukute aliyemkamata kakataa kutoa kitu kidogo (rushwa), bambika kosa mrundike huko au mmegongana vijumbani huko unamtafutia angle (kona) unambambikia kosa. Kesi 1,840 zimefutwa, hawa ni binadamu, hatujui wamekaa ndani kwa muda gani.

"Serikali inaendelea kulisha mahabusu, jamaa zao kutwa kiguu na njia kupeleka chakula, lakini wewe uliyefanya unasikia raha kabisa 'nimemkomesha yupo huko', umemkomesha we Mungu?

"Umemkamata hujapeleleza, umeambiwa tu huyo msweke ndani, huo ni mzigo kwa serikali na mzigo kwa familia yake. Sasa tuyaangalie vizuri haya matumizi ya nguvu, wanachotaka wananchi ni kuona haki ikitendeka kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo," Rais aliagiza.

**MKASA WA MBUGI**

Unaporejewa mkasa wa kijana Mbugi, mkazi huyo wa Mbagala wilayani Temeke mkoani Dar es Salaam, anasimulia namna alivyowekwa mahabusu kwenye Kituo cha Polisi Oysterbay wilayani Kinondoni kwa miezi mitatu katika mazingira ambayo anadai kuwa na harufu ya rushwa.

"Nimekaa mahabusu ya polisi kwa siku 89 (kuanzia Agosti mwaka jana). Kesi yangu dhamana ilikuwa wazi lakini sikupewa dhamana wala kupelekwa mahakamani kwa sababu sikuwa na laki tatu (Sh. 300,000) aliyotaka mpelelezi wa kesi yangu ili nipewe dhamana.

"Nilisingiziwa wizi wa bajaj, tulikamatwa vijana watatu, lakini wenzangu waliachiwa mapema tu kwa sababu walikuwa na fedha. "Sasa nimefanikiwa kutoka polisi kwa sababu nimeona ninazidi kuteseka na kupoteza muda, nikaamua niwaruhusu wazazi wangu wauze kiwanja changu ili ipatikane hiyo fedha, vinginevyo nisingetoka na mpelelezi wa kesi yangu alikuwa ananiambia nisipojiongeza nitafia mahabusu," anasema.

Hata hivyo, pamoja na utetezi huo, kutoa na kupokea rushwa ni kosa kwa mujibu wa sheria za Tanzania.

Kijana Mbugi anayezungumza kwa hisia kali, anaendelea na simulizi yake, akitamka: "Nimepoteza malengo mengi kwa muda niliokaa mahabusu. Sasa sijui wapi kwa kuanzia. Mke wangu amepata shida sana ikizingatiwa ana mtoto mdogo, wametaabika sana."

Kijana huyo anasimulia uzoefu wake wa miezi mitatu mahabusu kwamba kuna baadhi ya mahabusu wenzake aliwakuta huko na amewaacha wakiwa hawajui hatima yao.

"Nilipowekwa mahabusu, nilimkuta kijana mwingine ambaye sikujua aliingia lini na nilipotoka, nimemwacha humohumo na sijui atatoka lini," anasema.

**MKEWE ALONGA**

Mke wa Mbugi, Irene Kimbe anasimulia kilichojiri baada ya mumewe kuswekwa mahabusu, akisema: "Mume wangu kwa bahati mbaya siku alipokamatwa, ndani tulikuwa na fedha kidogo sana. Kuanzia hapo ilibidi nianze kumpelekea chakula kila siku kituoni.

"Nilimpelekea huku nikifuatilia mwenendo wa kesi yake kwa mpelelezi, majibu waliyokuwa wananipa yalikuwa yananikatisha tamaa lakini kwa sababu ninampenda mume wangu na niliamini katika Mungu sikukata tamaa, niliendelea kupeleka huduma kila siku.

"Baadaye ile fedha ikaisha na kituoni alikokuwa anashikiliwa ni mbali na hapa tunapoishi. Kuna wakati ilinibidi nitembee kwa miguu kupeleka chakula.

"Kuna muda mimi na mwanangu, tulikuwa hatuwezi kula chakula bila kuhakikisha tumeishampelekea chakula. Baada ya fedha kuisha, nilikosa namna ya kupata fedha, nikauza godoro, tukawa tunalala chini. Fedha iliyopatikana ilitusaidia kumhudumia na sisi angalau kupata chochote kitu.

"Na vitu vingine vingi vya thamani niliviuza ili mume wangu asikose chakula, pia nilihitaji nauli, kila siku nilikuwa ninatumia zaidi ya Sh. 4,000 kama nauli ya kwenda na kurudi," Irene anasimulia yaliyowasibu kipindi hicho wakiwa wakazi wa Tegeta wilayani Kinondoni.

**MKASA UNAOFANANA**

Kilichomsibu Mbugi kinashabihiana na mkasa wa Remi Kinusi, mkazi wa Mikocheni wilayani Kinondoni, aliyedai kukaa mahabusu ya Kituo hichohicho cha Oysterbay kwa siku 58.

"Nilisingiziwa kesi ya wizi wa kuaminika. Nikiwa nyumbani, walikuja askari na bajaj wakanikamata na kunipeleka kituo cha polisi na baada ya kufika huko, bila maelezo yoyote nikawekwa mahabusu.

"Nikakaa mahabusu kwa siku mbili ila kuhojiwa. Kila alipokuja mpelelezi wangu, nikimwambia kuhusu dhamana au kwenda mahakamani alikuwa ananiambia 'dhamana haitoki hivihivi', hata ndugu zangu walipokuja kwa ajili ya kuniwekea dhamna aliwakatalia.

"Nilikaa siku 58 mahabusu, siku niliyofanikiwa kutoka alikuja mkuu wa kituo akaniuliza 'imekuwaje upo humu ndani kwa siku zote hizo?' Nikamwambia 'mpelelezi wa kesi yangu hataki kunipa dhamana wala kuipeleka kesi yangu mahakamani'.

"Baada ya kunihoji, akachukua jina langu akaondoka nalo, baada ya muda kidogo nikaitwa, niakaambiwa nichukue kila kitu changu, kwamba nipo huru kwenda nyumbani," Kinusi anasema.

**HATUA SERIKALINI**

Nipashe ilipomtafuta kuzungumzia tuhuma hizo dhidi ya askari wake, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alisema:

"Hizo sheria zipo wazi, mtu mbaya wa kwanza anayetuharibia askari wetu ni mtoa rushwa, hao ndiyo wanatuharibia askari wetu, usipompa rushwa atapata wapi?

"Imefika wakati wa watu kutolitupia lawama Jeshi la Polisi dhidi ya rushwa, inabidi waangalie na upande wa mtoaji. Kama ameombwa rushwa, kwanini asitoe taarifa?

"Tukimkamata mtu anayetoa rushwa kwa askari wetu, tutamshughulikia kwa sababu huyo ndiye anatuharibia askari wetu, tunataka jamii iachane na hii dhana, hayo ni mambo ya kufirika."

**NENO LA TAKUKURU**

Taasisi ya Kuzuia Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kupitia Mkurugenzi wake wa Elimu Kwa Umma, Joseph Mwaiswelo inakiri kuwa na taarifa za madai ya askari wa jeshi hilo kunyoshewa vidole kuendekeza rushwa, ikianika mikakati iliyopo kukabili.

"Tunachokifanya ni kuendelea kutoa elimu kwa wanajamii ili waendelee kufahamu madhara ya rushwa kwa ujumla wake, tumebaini watu wengi wana uelewa mdogo juu ya madhara ya rushwa.

"Rushwa inaleta umaskini, inanyima haki na ni adui wa maendeleo kwa taifa letu. Sisi tunaendelea na operesheni zetu za kuwatafuta na tukiwabaini tutawapeleka kwenye vyombo vya sheria. Lakin ikumbukwe pia jukumu la kupambana na rushwa si la TAKUKURU pekee yake, bali ni jambo ambalo kila mtanzania anatakiwa kulibeba," anasema.

**JICHO LA KISHERIA**

Mratibu wa Mtandao wa Kutetea Haki za Binadamu,

INAENDELEA UK. 5

# Mwalimu mwenye ulemavu wa macho abuni mtambo wa kuzalisha umeme

**Na Thobias Mwanakatwe**

MWALIMU mstaafu ambaye ana ulemavu wa macho, George Rubagumya, amebuni mtambo wa kuzalisha umeme wa nishati jadidifu ambao utakuwa na uwezo wa kuzalisha wati 42,000.

Mtambo huo ambao ameupa jina la Injini ya Tanzanite, umeme wake unaweza kutoa huduma kwa kati ya nyumba 10 hadi 25 ambazo matumizi yake ya nishati hiyo ni ya kawaida.

Rubagumya ambaye anaishi Tabata Segerea jijini Dar es Salaam, akizungumza katika mahojiano na Nipashe, alisema utafiti wa teknolojia hiyo aliuanza mwaka 2018 katika harakati za kutafuta suluhisho la kudumu la mgawo wa umeme nchini.

Alisema kuwa teknolojia hiyo itasaidia kupunguza gharama za ujenzi wa miundombinu ya umeme zikiwamo nguzo.

Kwa mujibu wa Rubagumya, teknolojia hiyo inatumia mabomba maalum kutoka kwenye kisima ambacho kinachimbwa karibu na mtambo huo na kusukuma maji kwenda juu kwa nguvu kubwa na kurudi kwenye bwawa hilo.

Alisema kisima hicho kinajazwa maji lita 1,188 ambayo yanaweza kutumika kuendelea kuzalisha umeme kwa zaidi ya mwaka yakiwa ndani ya kisima hicho.

Mwalimu huyo alisema ujenzi wa mtambo huo ulianza rasmi Julai mwaka jana na umefanyika kwa kusuasua kutokana na ugumu wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kununua vifaa vya ujenzi.

Alisema kuwa hadi sasa ametumia Sh. milioni 4.2 kati ya Sh. milioni 14 zinazohitajika kukamilisha ujenzi wa mtambo huo. "Ni sawasawa na kusema teknolojia hii inalazimisha maporomoko ya maji sawasawa na umeme, haihitaji mto kujaa maji, mvua kunyesha wala upepo, iwe kiangazi umeme wake wa kutosha ukishajaza maji," alisema.

Mbunifu huyo alisema umeme wake unaweza kutumika ofisini, viwandani, hospitalini na kwenye makazi ya watu.

Akitaja faida ya teknolojia hiyo kuwa inakuhakikishia upatikanaji wa umeme wakati wote na mahali popote na pia mtambo huo mbali na kuzalisha umeme, pia unaweza kutumika kwa shughuli ya umwagiliaji mashamba.

Aliongeza kuwa mtambo huo hautumii nyaya, nguzo na vifaa vingine ambavyo vingetumia fedha nyingi kununua miundombinu.

Alisema ubunifu huo unafahamika kwa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) na Wizara ya Nishati lakini anashindwa kuukamilisha mapema kutokana na ukosefu wa fedha Sh. milioni 10 zinazohitajika kumalizia.

Alisema kuna kipindi aliwasiliana na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), wakamshauri kubunifu huo inabidi auwasilishe kwa taasisi zinazotambuliwa kisha taasisi hizo ndizo zipeleke suala hilo kwao.

Rubagumya aliwaomba wadau mbalimbali wajitokeze kumsaidia ili akamilishe ndoto yake hiyo ya kukamilisha ujenzi wa mtambo huo na uzalishaji kuanza mara moja.



Ujenzi wa barabara ya mabasi yaendayo haraka (BRT III), ukiendelea katika barabara ya Nyerere, Banda la Ngozi, Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Biteko aagiza kampuni madini ujenzi kuandaa mpango uwajibikaji kwa jamii

**Na Mwandishi Wetu,**
ARUSHA

WAZIRI wa Madini, Dk. Doto Biteko ameitaka Kampuni ya Madini Ujenzi ya Rocktronic Ltd inayochimba kokoto, kuandaa mpango wa huduma kwa jamii inayozunguka mgodi huo ili kuiwezesha jamii kunufaika na rasilimali madini iliyopo kwenye maeneo hayo.

Aliagiza hayo juzi alipotembelea machimbo ya kokoto eneo la King'ori unaofanywa na kampuni hiyo wilayani Arumeru mkoani Arusha.

Dk. Biteko alisema mpango huo utasaidia kuwa na malengo ya huduma kwa jamii ili kuleta maendeleo na kuondoa migongano inayoweza kujitokeza siku za baadaye na wakazi wa eneo hilo. Alisema mpango huo utasaidia katika kujenga uhusiano mzuri na jamii. Aliitaka kampuni hiyo kuandaa taarifa ya upembuzi yakinifu ili kuiwezesha kujua muda wa uhai wa mgodi, kiasi cha mashapo na kiasi kitakacholipwa kwa serikali.

Akizungumzia utunzaji wa mazingira, Dk. Biteko aliielekeza kampuni hiyo kuanza kupanda miti kwenye maeneno ya machimbo ili kuhifadhi mazingira. Alitoa wiki mbili za kuanza kupanda miti na kuitaka kampuni hiyo kuajiri ofisa mazingira.

Waziri huyo alisisitiza kampuni hiyo kuandaa mpango wa uchimbaji ili kuacha kuchimba kwa kuhama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine na kueleza kuwa mpango huo utasaidia kuwa na uchimbaji wenye tija na endelevu.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Rocktronic Ltd, Prajesh Chauhan alisema kuwa kampuni hiyo imefanikiwa kutoa ajira ndani ya Kata ya Malula kwa wazawa wenye ujuzi na wasio na ujuzi wapatao 118.

Alisema kampuni imechangia shughuli za maendeleo ndani na nje ya kata kwa kutoa vifaa mbalimbali kama vile kokoto, mawe, vifusi na fedha ili kusaidia miradi ya maendeleo ya wananchi katika sekta za elimu, afya, maji na barabara za ndani.

Ofisa Madini Mkazi Mkoa wa Arusha, Alphonce Bikulamchi alisema Ofisi ya Madini Arusha itaendelea kushirikiana na wadau wote ikiwamo ofisi ya Mkuu wa Wilaya Arumeru na Mkurugenzi Mtendaji wao kwa lengo la kuongeza ufanisi na tija katika shughuli za uchimbaji madini.

Alisema pia ofisi itaendelea kutoa elimu juu ya Sheria ya Madini Sura 123 na Kanuni zake pamoja na miongozo mingine ya Serikali ili kuchangia ukuaji wa Sekta ya Madini kwa ujumla.

## Simulizi ya kijana aliyekaa mahabusu ya polisi siku 89

INATOKA UK. 4

Onesmo Olengurumwa anasema kitendo cha kumnyima dhamana mtuhumiwa mwenye haki ya kupata ili kuweka mazingira ya kujipatia rushwa, ni ukiukwaji wa haki za binadamu na uvunjifu wa sheria.

"Ikiwa mtuhumiwa akiendelea kushikiliwa polisi kwa zaidi ya muda wa kisheria (saa 24), ndugu wanaweza kwenda mahakamani kufungua kesi ya haraka ya kumtoa mtu polisi ambaye amewekwa kinyume cha utaratibu na mara nyingi mahakimu huwa wanatoa sana kipaumbele kwenye kesi kama hiyo," anasema.

Wakili wa Kujitegemea kutoka Kampuni ya Accuracy yenye maskani yake Kinondoni mkoani Dar es Salaam, Bashiru Yakubu analitafsiri suala hilo ni kunyume cha sheria, akiwa na ufafanuzi kwamba askari anayezuia dhamana, anakuwa amefanya kosa kwa muujibu wa sheria.

"Sheria (ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai) inamtaka mtuhumiwa kukaa mahabusu ya polisi kwa saa 24 tu na katika muda huo jambo moja kati ya haya matatu liwe limeshafanyika - mtuhumiwa kuachiwa huru, kutoka kwa dhamana au kupelekwa mahakamani," Wakili Yakubu anafafanua.

Hata hivyo, sheria hiyo inaelekeza masharti hayo hayazingatiwi kwa mtuhumiwa wa jinai inayohusiana na adhabu ya kifo.

Wakili Yakubu anashauri elimu itolewe kwa askari wa Jeshi la Polisi, akidai kuwa wengi wao hawana taalamu ya sheria na haki za mtuhumiwa.

"Pili, ukiona una ndugu yupo kituo cha polisi kwa muda mrefu, inabidi upeleke malalamiko kwa Kamanda wa Polisi Mkoa, ikitokea ameshindwa kutoa msaada, basi nenda mahakamani.

"Kuna kitu kinaitwa 'hubiascoppus'. Haya ni maombi ambayo unayapeleka mahakamani unamshtaki Mkuu wa Kituo cha Polisi, RPC (Kamanda wa Polisi wa Mkoa), Mkuu wa Upelelezi Wilaya (OCD) pamoja na Mkuu wa Jeshi la Polisi, halafu unawapeleka mahakamani katika eneo ambalo mtuhumiwa anashikiliwa, maombi hayo huwa yanapewa kipaumbele cha kusikilizwa muda huohuo, shida ni kwamba wengi hawalijui hili. "Ukishaipeleka kesi hiyo mahakamani, ukawaambia kuna mtu yuko mahabusu amezuiliwa, hawataki kumpeleka mahakamani wala kuachiwa kwa dhamana, wakishaona wanaitwa mahakamni kwa kesi hiyo, mtuhumiwa ataachiwa muda huohuo.

"Na ukimkuta hakimu mahakamani hata kama muda wake umekwisha, lazima atawapa hati ya wito na atawasubiria mpaka mtakaporudi, hapo ndipo mahakama itajua kama mtuhumiwa ana haki ya kupata dhamana au la.

"Uzoefu unaonyesha kuwa mara nyingi wakishaona suala limefika mahakamani, huwa wanamwachia mtuhumiwa hapohapo. Mimi nina kesi nyingi ambazo zimeisha kwa namna hiyo," Wakili Yakubu anahitimisha ufafanuzi wake.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# MSD inapaswa kujitafakari madai utendaji wake wa kazi

**KWA** miaka ya hivi karibuni, Bohari Kuu ya Dawa (MSD) imekuwa ikilalamikiwa kwa utendaji mbovu hatua ambayo imesababisha mara kadhaa baadhi ya watendaji waandamizi wa taasisi hiyo kuchukuliwa hatua, zikiwamo za kinidhamu.

Tangu kuanza kwa uongozi wa serikali ya awamu ya tano chini ya Hayati Dk. John Magufuli, watendaji mbalimbali wakiwamo wakurugenzi wakuu, wameondolewa kutokana na madai ya kutokutekeleza wajibu wao ipasavyo. Licha ya kuondolewa kwenye nyadhifa zao, baadhi ya wakurugenzi wakuu hao na wakuu wa idara, wamefikishwa katika vyombo vya dola kwa uchunguzi kutokana na tuhuma mbalimbali zikiwamo za ubadhirifu.

Mbali na kuchukuliwa hatua hizo, viongozi wa ngazi za juu serikalini kila wanapofanya ziara kwenye maeneo mbalimbali ya nchi, wamekuwa wakipokea malalamiko ya utendaji wa idara hiyo nyeti katika afya, yakiwamo ya kukosekana kwa dawa na vifaa tiba kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Madai hayo pamoja na tuhuma za ubadhirifu, vimesababisha baadhi ya watendaji kutimuliwa, kwa lugha maarufu kutumbuliwa huku viongozi wakitoa matamko ya kutoridhishwa na utendaji wa taasisi na kutaka watumishi wake wabadilike.

Pamoja na matamko hayo na hatua zilizochukuliwa dhidi ya maofisa waandamizi, utendaji mbovu au usioridhisha ndani ya MSD sasa umeonekana kuwa donda ndugu au mfupa mgumu uliomshinda fisi.

Hilo limebainika baada ya juzi Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi kuonyesha kuchukizwa na utendaji kazi mbovu wa idara hiyo iliyopewa kazi ya kuagiza, kuhifadhi na kusambaza dawa na vifaa tiba kwa niaba ya serikali kwa ajili ya vituo vya serikali vya kutolea huduma za afya.

Prof. Makubi alifikia hatua hiyo baada ya malalamiko kwamba MSD imeshindwa kufikisha dawa muhimu katika vituo mbalimbali vya afya na kusababisha madeni. Kutoana na hali hiyo, Katibu Mkuu huyo aliipa MSD miezi miwili kuhakikisha tatizo la kukosekana kwa dawa linamalizika ndani ya miezi miwili.

Katibu mkuu alifikia kueleza hayo jijini Mwanza alipoelezwa na wadau kuwa hali ya upatikanaji wa dawa muhimu katika vituo vya kutolea huduma za afya imekuwa ngumu kutokana na taasisi hiyo kushindwa kufikisha dawa kwa wakati. Alishangazwa kuona kwamba hospitali na vituo vya afya vimelipa fedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa hizo wakati MSD ikiwa haijatekeleza.

Alitoa agizo hilo juzi jijini Mwanza wakati akizungumza na wadau na viongozi mbalimbali wa afya juu ya uboreshaji wa huduma ya afya kwa wananchi sambamba na utekelezaji wa bima ya afya kwa wote unaotarajiwa kuanza Julai 2023.


Profesa Makubi alisema MSD wamesababisha hali ya upatikanaji wa dawa muhimu unakuwa mgumu hasa katika vituo vya serikali na kuwalazimu kufuata dawa nje ya vituo ilihali tayari vituo hivyo vimelipia gharama kubwa za kuagiza dawa kwao lakini bado idara hiyo haipeleki dawa katika vituo kwa wakati.

Jambo ambalo lilimshangaza Katibu Mkuu ni kwamba vituo vya kutolea huduma za afya vimeshalipa fedha tayari MSD lakini imeshindwa kutekeleza mkataba wa kusambaza dawa kwa mteja. Hapo ndipo kwenye ukakasi na kusababisha kuwapo kwa maswali mengi bila majibu.

Kutokana na malalamiko hayo, ni vyema MSD ikajitafakari utendaji wake katika kutekeleza majukumu yake, vinginevyo ikubali kwamba imeshindwa kazi ili serikali itafute mbinu nyingine bora ambayo itasaidia wananchi kupata huduma kwa haraka.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Shule zinapoanza mtoto asiwe hapa



Na Sabato Kasika

**SHULE** za msingi na sekondari zinafunguliwa kuanzia kesho suala la kusoma, kufurahia masomo katika mazingira mazuri pamoja na kufaulu ni kipaumbele, lakini usalama wa watoto na ulinzi wao ni jambo linalohitaji wazazi,walezi na jamii kulipa umuhimu wa kipekee.

Ulinzi na usalama unagusa kila mmoja kuwaangalia kuanzia shuleni wanaposoma , mitaani wanapokaa na mambo muhimu wanayohitaji ili kuwasaidia wasome salama.

Lakini juhudi hizi ziende pamoja na kuhakikisha kuwapo kwa huduma za kijamii kama maji, chakula na mabweni shuleni maana vitu hivyo vinapokosekana huleta shida hasa kwa mabinti.

Ni kwa sababu watoto wengi wanaoathirika na ukatili wa kijinsia hasa mabinti kupewa mimba utotoni, kutumiwa kingono na walimu au walezi na hata kuozwa kunaweza kuchangiwa na ukosefu wa huduma za jamii.

Ukiangalia zaidi eneo la sekondari, huduma muhimu zinazozungumziwa hapa ni kama chakula, mabweni, maji, hospitali na usafiri.

Kwa kiasi fulani ukosefu wa bweni huwalazimisha wasichana kupanga nyumba mitaani, wakati kuishi bila maji kunachangia kujihimu alfajiri kwenda kisimani au mtoni au usiku wa manane kusaka maji yote yakiwatumbukiza kwenye mikono ya wanyanyasaji.

Kusoma pasipo na chakula kunamaanisha njaa isiyovumilika, matokeo yake ni binti kufanya lolote bila kujali itakuwaje ili apate chakula, asife njaa. Yote hayo na mengine mengi huchangia mimba, utoro na watoto kuchukia shule.

Ni vyema wazazi, walezi na wadau wa elimu watatue matatizo hayo yanayohusiana na huduma za msingi ili kupunguza tatizo linalohusiana na kukwamishwa kusoma kutokana na matatizo hayo kila mwaka.

Usalama na ulinzi wa watoto unakwenda mbali zaidi kwa kuwasimamia na kuwaepusha na athari za utandawazi ni kwa sababu umewaharibu watoto wa sekondari na msingi kwa vile wamekuwa wateja wa mitandaoni kujifunza'maovu.'

Wanatumia simu kuangalia picha kwenye YouTube zenye maudhui ya ngono, kujifunza masuala mengine makubwa kuliko umri wao, wapo wanaojifunza na kufanya uhalifu.

Utandawazi unawatumbukiza katika kupenda muziki wa disko usiku, lakini wale wanaokaa mbali na nyumbani au waliopanga mitaani ni wapenzi wa mikesha ya harusi na ngoma.

Wakati mwingine ni waraibu wa sinema zinazoonyeshwa kwenye vibanda umiza mitaani.

Watoto hawa wanapokosa uangalizi wanaweza kuishi kwenye nyumba za sinema mchana au vibanda umiza, mabinti wanaweza kuzamia kwenye mikesha au wakaranda mitaani kwa maelezo kuwa hakuna mabweni shuleni wanalazimika kupanga.

Wengi huishia kushawishiwa na kutumbukia kwenye vitendo vya kuwakwamisha kimasomo.

Watoto wanaingia mitegoni wanapokwenda kwenye mabanda yanakoonyeshwa video mchana na kukutana na watu wanaowalipia kiingilio, kuwapa chips na soda kitakachofuata ni ulaghai na hadaa za ngono, zinazoweza kuwaondoa shuleni, kupata mimba na kuzitoa utotoni na kuambukizwa magonjwa.

Pamoja na udanganyifu huo mabinti wanaweza kuingizwa mtegoni na walimu ambao ama kwa kisingizio cha kuwafundisha twisheni au kuwaomba wasaidie kazi za nyumbani wanawabaka au kuwashawishi kuingia kwenye ngono.

Ni vyema kuwaangalia watoto wasiwe waathirika wa kutafuta fedha za kujikimu kwa kulazimishwa kufanyakazi za kuosha vyombo, kutafuta kuni , kufua nyumbani kwa walimu na wanavijiji au wanajamii ili kupata fedha za kuishi na kununua mahitaji ya msingi ya kitaalamu na maisha.

Wazazi, walezi , jamii na asasi za kiraia waanze kufuatilia na kuhoji sababu za wasichana au wanafunzi kuzurura, kufanya mambo yanayokwenda kinyume na taratibu.

Mambo yasiishie hapo taarifa zifikishwe polisi, dawati la jinsia, kwa watendaji wa elimu na hata viongozi wa siasa ili kupata ufumbuzi.

Jamii isikae kimya maana kudhalilisha watoto hakuwezi kukoma kama jamii itaendelea kukaa kimya.

SAFU

FIKRA MBADALA

# Asante Mama kwa kuruhusu mikutano



Pascal Mayalla

JUNI 8, 2021 katika safu hii, niliandika makala ya kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwasisitiza watendaji wa serikali kutenda haki kutokana na baadhi ya haki zilizotolewa na Katiba yetu kugeuzwa ni hisani.

Leo tena, nampongeza Rais Samia baada ya kuruhusu mikutano ya siasa. Sasa ni nderemo na vifijo nchi mzima. Nikiwa Mtanzania mzalendo wa taifa letu, pale linapofanywa jambo jema lolote la kheri kwa mustakabali mwema kwa taifa letu, sina budi kujiunga na wengine wote wanaolitakia mema taifa hili kwa kumpongeza Rais wetu. Rais ameruhusu mikutano ya siasa, kukubali kurekebisha sheria mbalimbali kandamizi na kubwa kuliko, kukubali kuendeleza mchakato wa Katiba mpya.

Mikutano ya hadhara kwa vyama vya siasa ni jambo ambalo limeruhusiwa na katiba, hivyo kufanya mikutano ni miongoni mwa haki zilizoainishwa. Hata lile swali langu la Ikulu, kumwuliza Rais (Hayati) John Magufuli ametumia mamlaka gani kwenye kifungu kipi cha sheria kuzuia jambo lililoruhusiwa na katiba japo sikumbuki nilijibiwa nini, lakini sasa ndiyo Rais Samia amemjibia.

Waswahili wana msemo, "anayekuja pasi na hodi, huondoka pasi kuaga". Jambo linalozuiwa kwa utashi tu bila kifungu chochote cha katiba au sheria, sasa limeruhusiwa kwa utashi tena bila kutumia kifungu chochote cha katiba na sheria. Jambo lolote lililozuiwa, linaporuhusiwa, hatua ya kwanza ni kushukuru, hivyo Watanzania wote tuungane na kusema kwa kauli moja kusema 'Asante Sana Mama'.

Sasa twende ndani kidogo zaidi ya jambo lenyewe lililoruhusiwa. Kwa vile mikutano ya siasa ilizuiwa kwa utashi tu na sasa imeruhusiwa kwa utashi tena, tukishukuru na kusema tu asante bila kutia neno jingine lolote, itaonekana suala la mikutano ya siasa ni kama jambo la hisani tu ya Rais aliyeko madarakani.

Rais wa awamu ya tano, Dk. John Magufuli, alizuia mikutano kwa utashi tu na leo Rais Samia ameruhusu mikutano hii kwa utashi na kwa hisani tu. Tusipoliwekea mwongozo suala hili, kesho atakuja kiongozi mwingine naye atazuia jambo lolote kwa utashi tu.

Kitu kama ni haki, ni stahili si hisani. Je, sisi Watanzania tutaendelea kuruhusu viongozi wetu, wazigeuze haki zetu na stahili zetu kuwa hisani mpaka lini?

Tena afadhali ya hili la haki ya mikutano ya siasa, limefanywa kwa utashi tu kwa kutumia kauli tu. Mikutano ilizuiwa kwa kauli na sasa imeruhusiwa kwa kauli. Lakini kuna na haki nyingine mbili ambazo ndizo haki kuu za kiraia zilizotolewa na katiba yetu. Haki hizo ni haki za kuchagua na kuchaguliwa, moja kati ya haki mbili hizo, imegeuzwa hisani. Haki ya kuchagua yenyewe bado ipo ila haki ya kuchaguliwa imegeuzwa hisani.

Tunamshukuru sana Rais Samia kutuhisania Watanzania kuturudishia haki hii. Tuendelee kumwombea Rais Samia Mungu aendelee kumlinda na kumbariki ili kufikia mwaka 2025, awe ameisha turudishia haki zote za kikatiba zilizoporwa na kugeuzwa hisani. Nimeutaja mwaka 2023 japo ninaelewa Rais Samia anayo fursa ya kuendelea kuhudumu kipindi cha pili cha mwaka 2025-2030. Mimi natumia mtindo wa linalowezekana leo lisingoje kesho. Sasa tuko 2023, tujipange kukamilisha yote ya msingi, akiendelea, aendelee na mengine wakati ya msingi yamekamilika.

Watanzania tuendelee kuwa watu wa shukrani kwa kushukuru kwa yote hata kama ni madogo ili tupatiwe makubwa. Kwa hiyo tuendelee kusema asante sana Mama Samia kwa utashi mzuri wa kisiasa wa kuruhusu mikutano ya siasa. Kwa utashi huu, vyama na Watanzania tukushukuru kwa hisani yako hii, tunakuomba tumia utashi wa kisiasa huu huu kuwaruhusu Watanzania wote kuchagua na kuchaguliwa.

Wakati tukisubiri hisani ya Mama Samia kwenye hili, kupitia marekebisho ya sheria mbalimbali na kumruhusu kila Mtanzania kuchagua na kuchaguliwa, naendelea tu kukumbushia kuwa haki ni stahiki si hisani, haki haiombwi na kutegemea hisani, wala haki haihitaji vikao.

Mikutano na majadiliano na maridhiano kuzijadili haki na haki hauletewi kwenye kisahani cha chai kama hisani, fadhila au zawadi, haki ni stahiki inayopaswa kutolewa unconditional bila masharti yoyote. Haki inapaswa kutolewa bila masharti yoyote. Haiombwi wala haibembelezewi kwa vikao vya maridhiano bali hudaiwa na katika kuidai huku kukishindikana kuidai kwa amani na kisheria, ndipo nguvu hutumika kuipigania, kwa kuweka mashinikizo ya mikutano na maandamano. Hapa ni pale tu inapobidi, baada ya njia nyingine zote kushindikana. Ni katika kuipigania huku, kuna wakati machozi, jasho na damu huweza kumwagika.

Kwa vile Rais wetu kashaonyesha utashi, kwa kauli na matendo, tuzidi kumwombea ili Mungu amwezeshe ayaweze yote haya kabla hajamaliza awamu yake hii ya kwanza. Hata ikitokea akaendelea kwa awamu ya pili, hiyo itakuwa awamu ya shukrani na kumpa asante kwa aliyotatenda na si awamu ya kukamilisha ambayo hayakukamilika.

**Mungu Mbariki Rais Samia**
**Mungu Ibariki Tanzania**
**Pascal Mayalla**
**+255 754 270403**

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Shukurani zetu kwa Samia zijidhihirishe kwa vitendo



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

HERI ya Mwaka Mpya tena mpenzi msomaji wa safu hii! Hongereni sana Watanzania wenzangu kwa kuuona mwaka mpya na kupokea zawadi ya aina yake kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Hakika ni zawadi ya aina yake, aliyoitoa hivi karibuni Ikulu ya Magogoni alipozungumza na vigogo wa vyama vya siasa nchini. Si nyingine bali ni ile ya tamko la kuondoa marufuku ya mikutano ya hadhara ya kisiasa.

Lakini pia uamuzi wa kupitia sheria mbalimbali na kuzifanyia marekebisho kama si kuziondoa, pamoja na kukwamua mchakato wa Katiba mpya uliokwama mwaka 2014. Tumshukuru sana Rais kwa hilo.

Uongozi ni karama kutoka kwa Mwenyezi Mungu na hii ndiyo aliyopewa Rais Samia kwamba anaangalia maslahi mapana ya Watanzania wote badala ya kukumbatia itikadi kama ilivyokuwa kwa mtangulizi wake, aliyepata kusema maendeleo kwa wapinzani hayastahili.

Ikumbukwe pia wasifu wa mtu na uzoefu wa nyuma humwezesha kuongoza watu kwa kufuata njia nzuri au mbaya kimaisha. Watanzania tumeshuhudia haya kwa mifano hai kabisa.

Rais Jakaya Kikwete katika maisha yake ni mtu wa kuchanganyika na wengine kwani hata kabla ya kuwa kiongozi wa nchi alidiriki kwenda vijiweni Kariakoo na kukaa na wazee na vijana, aghalabu akifikia hata kuingia kwenye dansi la bendi ya Mlimani Park na kuwa mmoja wa mashabiki wake kindakindaki.

Akiwa waziri, hususan wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Kikwete aliiwakilisha nchi vizuri sana kimataifa na heshima yake ya tangu enzi za Mwalimu Julius Nyerere kudumu, akifanya hivyo hata alipokuja kuwa mkuu wa nchi.

Aliendelea kuchangamana na watu wa kaliba tofauti wazee kwa vijana, wanaume kwa wanawake, hakuchelea kukaa na vijana wakiwamo wasanii kubadilishana mawazo na wakati mwingine akiwasaidia 'kutoboa'. Alifanya hivyo hata kwa wanasiasa bila kujali itikadi.

Akaja Dk. John Magufuli, ambaye aliona sera ya kimataifa kama anasa huku akikataa kusafiri kimataifa si yeye tu hata kwa wasaidizi wake, akisema ni gharama na matumizi mabaya ya fedha za umma. Tanzania kimataifa ikachechemea.

Lakini kabla ya kuwa mkuu wa nchi, alifanya vizuri akiwa Waziri wa Ujenzi akijenga barabara nchi nzima. Wasifu na mazoea hayo akayadhihirisha aliposhika ukuu wa nchi ambapo alijikita zaidi kwenye ujenzi wa barabara, viwanja vya ndege, kuta, madaraja na reli.

Rais Samia kama ijulikanavyo, ana historia ya kuwa mwanaharakati aliyejihusisha sana na utetezi wa haki za binadamu, huku akishirikiana na wanawake kutetea haki sawa na kuwasaidia katika mambo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa. Ilifikia hatua akaitwa 'Bibi Mchele' kutokana na misaada yake kwa binadamu wenziwe.

Hakuishia hapo, aligombea ubunge ili akapambane na mawaziri waliokuwa wakisema uongo kwa wananchi, lakini bahati isiyo yake, alipoingia bungeni akapewa uwaziri na hivyo badala ya kuhoji wasema uongo yeye akajikuta anahojiwa.

Kwa kuwa mtangulizi wake alijikita katika miundombinu na kuzuia siasa, akidhani siasa haiendani na uchumi, yeye alijikita katika maslahi ya watu na ndicho anachokionesha sasa, kwa kukutana na wanasiasa wote na kusaka maridhiano kwa mustakabali mwema wa nchi.

Kwa hiyo historia inaweza kukuletea kiongozi mzuri au mbaya, kutegemea na maono aliyo nayo, mtazamo wake wa kimaisha lakini pia dhana aliyonayo katika kujenga Taifa. Hapo ndipo tunapoweza kuwatofautisha, Kikwete, Magufuli na Samia na hatimaye kushukuru kuwa kudra za Mungu zilituletea Samia na anafanya yanayostahili kufanyiwa binadamu.

Shime Watanzania Samia amefungua tena mlango wa siasa, tutoke tukatumie fursa hiyo vizuri kama alivyoasa, tutumie mikutano ya hadhara si kutukanana, bali kupeana mipango, sera na miongozo chanya kwa Taifa.

Ni dhahiri tutasikia mengi kutoka kwa wanasiasa, yatakuwapo ya kweli na ya uongo. Ya uongo yawajibishwe na ya kweli yathibitishwe, ili majukwaa ya siasa yasitumike kuchafuana, kwa sababu tu ya kutaka kutinga Ikulu.

Kwa baadhi yetu, kauli ya Samia inaweza kuwa sawa na kutoa jini kwenye chupa iliyofungwa muda mrefu, kwani inaweza kutushuhudisha vituko na kauli za kichefuchefu, huku tukishindwa kulirejesha tena kwenye chupa.

Ili kudhihirisha shukurani za dhati kwa alichokifanya Rais Samia, Watanzania tujione ni wamoja tunaojenga nyumba moja kwa maslahi mapana ya Mama Tanzania, hivyo tusinyang'anyane fito ili hatimaye tukamilishe nyumba yetu na kuishi ndani yake kwa usalama, amani, upendo na mshikamano.

**Alamsiki!**

# Wanafunzi wa vyuo waitwa vita mabadiliko tabianchi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MKURUGENZI wa Idara ya Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais amewataka wanafunzi wa vyuo nchini kuwa mstari wa mbele katika utekezaji wa shughuli mbalimbali za kuhifadhi na kulinda mazingira ili kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

Dk. Andrew Komba alitoa rai hiyo jana aliposhiriki usafi wa mazingira kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma ulioandaliwa na Jumuiya ya Wanafunzi Taasisi za Elimu ya Juu (TAHLISO).

Mkurugenzi huyo aliyemwakilisha Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Dk. Switbert Mkama, alisema kazi hiyo ya usafi ni sehemu ya kuunga mkono utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021.

Aliwapongeza wanafunzi hao wa vyuo kwa kuandaa shughuli hiyo ya usafi ili kuunga mkono juhudi za serikali za usafi na uhifadhi wa mazingira ambapo kuanzia Januari 10 mwaka huu kutakuwa na upandaji miti katika Jiji la Dodoma.

"Kama mnavyofahamu serikali ilishautenga Mji wa Dodoma kuwa wa mfano katika masuala ya mazingira, hivyo tunahakikisha tunapanda miti ya kutosha na ninyi hapa leo (jana) mmeonyesha mfano kwa kufanya usafi hospitalini hapa," alisema Dk. Komba.

Mkugenzi huyo aliongeza kuwa ni wakati mwafaka kwa wanafunzi wa vyuo kuwarithisha wadogo zao njia za kutunza mazingira kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Mkuu wa Idara ya Afya Mazingira Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, Paul Mageni alisema kuwa katika kuiunga mkono serikali, wameanzisha bustani ya miti kwenye eneo la hospitali hiyo.

Mageni alisema miti iliyopandwa mbali ya kuhifadhi mazingira, pia inawasaidia wananchi wanaoapata huduma hospitalini hapo kupata hewa nzuri na matunda.

Viongozi wa TAHLISO kutoka Tanzania Bara na Zanzibar walitoa pongezi kwa uongozi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma kwa kuwapa wasaa wa kufanya usafi kwenye eneo hilo.

Pia waliwapongeza wanafunzi wa vyuo mbalimbali walioshiriki katika usafi, wakisistiza ni njia mojawapo ya kuiunga mkono serikali katika kuhakikisha mazingira yanakuwa endelevu kwa mustakabali wa taifa.

# Serikali yafanya mapitio kwenye matumizi ya bando

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

Serikali imesema inafanya mapitio upya kuona namna ambavyo itasaidia kupunguza gharama ya kutumia bando kubwa ili mwananchi wa kawaida apate huduma bila tatizo.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye alibainisha hayo jana alipozindua mnara wa Kampuni ya Mawasiliano ya Vodacom Tanzania kwenye Kijiji cha Kinenulo, Kata ya Imalinyi mkoani Njombe.

"Ni kweli Tanzania ukilinganisha na nchi zinazotuzunguka, gharama yetu ipo chini lakini gharama kuwa chini siyo kigezo peke yake, unaangalia na uwezo wa watu wanaotumia huduma.

"Kwa kulizingatia hilo na kwa kuzingatia ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi, tumetakiwa tuwafikie zaidi ya asilimia 80 ya watanzania.

"Kujenga mnara ukasimama hapa, kama mtu hawezi kuutumia itakuwa haina maana ndiyo maana tunapitia upya tuone namna ambayo huduma hizi zitawezekana hata mtu wa kawaida kabisa ambaye kipato chake ni kidogo kabisa awe na uwezo wa kuzitumia hizi huduma. "Kwa hiyo, niwahakikishieni tunauzindua mnara, baada ya uzinduzi mwisho wa mwezi huu tutaangalia tathmini ikiwa imekamilika mwishoni mwa mwezi huu tutatangaza bei mpya ya huduma za data ili kila mtanzania aweze kupata huduma hizi," aliahidi.

Nape pia kuwa wanatafuta namna ya kumwezesha mtanzania wa kawaida kumudu gharama ya kununua simu janja.

**SIMU KWA MKOPO**

Waziri huyo alisema kuwa kwa sasa wanafanya mazungumzo na kampuni za simu ili zitolewe kwa wananchi kwa mkopo, akifafanua: "Na mimi kwa sababu ninaipenda kazi yangu, nimeshaanza kuhangaika, tumebanana na kampuni za simu tunatafuta utaratibu ambao kampuni za simu na watoa huduma wengine wataleta simu walau iwe ni kwa mkopo, mtu alipe taratibu lakini aipate huduma aanze kutumia.

"Maana yake mtu wa kawaida kuchukua laki tatu (Sh. 300,000) ukaenda kununua simu, kidogo ngumu lakini tukimwambia weka elfu 30,000 upewe simu ya laki tatu halafu utakuwa unakatwa kidogo kidogo, hata kama ni kwa mwaka mzima, huduma unapata, umepata kwa bei ndogo na maisha yanaendelea, maagizo hayo ameyatoa Rais Samia."

Alisema endapo kila mtanzania atakuwa na simu janja, biashara itakua, kodi zitalipwa vizuri na huduma zitafanyika.

"Kwa hiyo ni matumaini yangu kuwapo kwa miundombinu ya mawasiliano kutaendana na kuwapo na vifaa vya mawasiliano na kutaendana na urahisi wa kuwasiliana," alisema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Mawasilino kwa Wote (UCSAF), Justina Mashiba alisema wana jukumu la kupeleka huduma za mawasiliano vijijini na tayari wamejenga minara 1,087.

"Mkoa wa Njombe tuna miradi 32, minara 32 katika hiyo minara 30 imekamilika na miwili ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na ruzuku iliyotolewa na serikali kupitia mfuko wetu ni Sh. bilioni 4.8," alisema Mashiba.

Kaimu Mkuu wa Kanda Nyanda za Juu Kusini wa Vodacom Tanzania, Magreth Lawrence alisema mnara huo wa kidijitali ulijengwa mwaka jana na ulianza kufanya kazi hivyo wamejizatiti kuhakikisha huduma ya mawasiliano inapatikana.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka alimweleza Waziri Nape kwamba Halmashauri ya Wanging'ombe inakabiliwa na changamoto ya kukosekana ofisi ya Posta.

Diwani wa Imalinyi, Onesmo Lyandala aliishukuru serikali kwa kutatua changamoto ya mawasiliano ambayo ilikua ikiwakabili na kwamba maendeleo yatakwenda kwa kasi.

Mmoja wa wakazi wa Kijiji cha Kinenulo, Veronica John alisema uzinduzi wa mnara huo utawasaidia kurahisisha shughuli za mawasiliano ambapo awali walikuwa wakilazimika kufunga safari ndefu kutafuta mtandao.



Barabara iliyopo nyuma ya Soko la Buguruni, Dar es Salaam, ikiwa imetuama maji ya mvua zilizonyesha hivi karibuni na kusababisha kero kwa watumiaji wa barabara hiyo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waajiri wabanwa usalama katika mazingira ya kazi

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

KAIMU Mkurugenzi wa Huduma za Biashara wa OSHA amewataka waajiri wote nchini kuweka mazingira salama ya kufanyia kazi ili kuendana na sheria za ndani na kimataifa.

Netiwe Mhando alitoa maagizo hayo jana alipozungumza katika kikao cha majadiliano baina ya Wizara ya Maliasili na Utalii na wadau wa Sekta ya Utalii.

OSHA ilikuwa miongoni mwa taasisi za serikali zilizoalikwa katika kikao hicho kwa ajili kusikiliza na kutolea ufafanuzi kero zinazowakabili wadau zinazohusu utekelezaji wa Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi ya Mwaka 2003 pamoja na kanuni zake.

Kaimu Mkurugenzi huyo alisema katika mkutano wa 110 wa kimataifa wa masuala ya kazi uliofanyika mwezi Juni mwaka jana, Geneva, Uswisi, suala la afya na mazingira salama ya kazi liliainishwa kuwa miongoni mwa haki za msingi za mfanyakazi mahali pa kazi.

Kutokana na maazimio hayo, nchi zote ambazo ni wanachama wa Shirika la Kazi Duniani (ILO), ikiwamo Tanzania, zinatekeleza mkataba wa kimataifa namba 155 unaozitaka serikali katika nchi wanachama kuwa na utaratibu na sera ya kitaifa ya usimamizi wa masuala ya usalama na afya mahali pa kazi. Alisema OSHA imejipanga kushughulikia kero zilizoainishwa na wadau wa sekta ya utalii na sekta nyingine likiwamo suala la ratiba za ukaguzi kutojulikana na hivyo kuathiri utoaji huduma. Alisema wadau hao watakaguliwa kupitia mpango wa ukaguzi wa kisekta.

"Msimu ujao wa ukaguzi wadau wa utalii watakaguliwa kwa wakati mmoja katika kipindi ambacho hakina watalii wengi na hivyo kuwawezesha kukidhi viwango vya usalama bila kuathiri biashara zao," alisema Mhando.

Kaimu Mkurugenzi wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi wa OSHA, Dk. Jerome Materu alisema taasisi hiyo inafanya jitihada kubwa katika kutekeleza andiko la serikali la uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji nchini (Blue Print) ambapo miongoni mwa hatua zilizochukuliwa na OSHA ni pamoja na kuondoa tozo zaidi ya 11 zilizoonekana kuwa kero kwa wafanyabiashara na wawekezaji nchini.

"Baada ya kuondoa tozo, sasa tunakwenda kwa wadau kupitia majukwaa mbalimbali kama haya kwa ajili ya kufahamu changamoto zinazowakabili katika kutekeleza taratibu za usalama na afya mahali pa kazi ili tuweze kuzitatua na hivyo kuendelea kuhamasisha uzingatiaji wa masuala ya usalama na afya kwa maendeleo endelevu ya taifa letu," alisema Dk. Materu. Kiongozi huyo alisema kuwa katika kipindi hiki ambacho Tanzania imekuwa ikipokea watalii wengi, kuna haja wadau wa sekta husika kuwekeza katika masuala ya usalama na afya ili kukidhi vigezo mbalimbali vya kimataifa na hivyo kuendelea kuwavutia wageni wengi zaidi kuja nchini.

# MAISHA

JANUARI 8, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*



Ukurasa 14


## Mexican Sosi na chapati za maji

## MAISHA NI NYUMBA

Ukurasa 15

Njia za kupendezesha meza ya chakula






## KATUNIKA


Ukurasa 16




# JIPODOE NYUMBANI

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | P | E | N | D | O |
| ■ | A | ■ | ■ | A | ■ |
| U | G | A | ■ | N | ■ |
| ■ | A | ■ | U | D | A |
| ■ | W | ■ | ■ | I | ■ |
| S | A | N | D | A | ■ |

## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
UMA, BEI, WANGA, DUNDA, DEREVA, DUMAZA

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI

HAYA, TAFUTA NJIA



## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

Mazungumzo kati ya marafiki wawili yalikua kama ifuatavyo;

Juma: Habari yako kijana?

John: Safi tu nambie,

Juma: Muda kweli naona unahangaika kumwagilia maziwa juu ya mikate, kwani ina matatizo?,

John: Nataka iwe laini kama ile ya dukani aliyonunua baba , akaniambia eti ni mikate ya maziwa.

Juma: Hapo unaharibu, ile inawekwa maziwa katika ngano na kisha inaokwa ikiwa na maziwa ndani na sio kumwagilia kama wewe.

SWALI

Tunda la fenesi kuna nini ndani yake?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Roho maalum zinazorudisha watu wengi kuwa wa zamani

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na mada zetu. Bado tupo katika kuufurahia mwanzo wa mwaka mpya wa 2023. Wiki iliyopita nilijadili siri unayopaswa kujua mwaka huu, nikataja eneo moja la kubadili mavazi.

Nikasema mwaka huu mpya watu hawapaswi kuwa vile vile kama walivyokuwa mwaka jana. Unapaswa kubadili tabia, mwelekeo, mtizamo, mfumo wa maisha, marafiki wasio na tija kwako na kadhalika.

Wengine bado wanaendekeza matambiko na maagano ya mababu ambao leo hii hawapo, jambo ambalo linawatesa wengi pasipo wao kujua. Mwisho wa mwaka zipo familia hukusanyika kijijini kwao kwa sherehe na wengine hutumia fursa hiyo kufanya matambiko. Yapo mambo hufanyika yakawa ni chukizo mbele ya Mwenyezi Mungu.

Zipo roho huruhusu watu kuingia mwaka mpya, lakini tabia au shida ni zile zile. Na kibaya zaidi ziko roho maalum za kuzimu zinawarudisha kuwa wa zamani. Ni ukweli usiopingika kwamba baadhi ya mababu zetu walikuwa waovu sana.

Wengi waliabudu miungu na waliweka maagano mazito na kutamka maneno mengi mazito juu ya uzao wao! Pia wako wengi wao walilaaniwa. Isitoshe, ziko baadhi ya kaya ambazo hadi leo wanaabudu miungu, hawataki kuachana na mambo ya asili ambayo hayana faida kwa maisha ya leo. Ukweli ni kwamba kama hutajitenga na mizimu kwa maombi ya hatari, unaweza kupata maadhara makubwa sana!

Cha ajabu ni kwamba roho hizi za mizimu zinaweza zisikuzuie kufanikiwa na kufikia kiwango cha juu kabisa. Lakini zenyewe zinahakikisha zinakushusha chini kabisa ili usipate nguvu ya kuinuka tena. Hasa wale wanaoingia kwenye wokovu ndio kabisa anguko lao huwa kubwa kwa kuwa huipiga vita mizimu na maagano yaliyowekwa na mababu zao.

Watu wengi sana leo ambao walitakiwa kuwa juu, wanaomba chakula kwani roho za mizimu zimewashikilia zikifuatilia nyendo zao zote. Siku Mungu akikufunulia uovu ulioko katika ukoo wako, utaomba kama hujawahi kuomba kabisa Mungu akuepushe.

Msomaji wangu, usidanyanyike kwani mizimu haina mpango wowote mzuri juu ya maisha yako. Hata kama ufanyeje, mizimu hufanya juu chini kuvuruga maisha yako! Mizimu huhakikisha wanatengeneza kalenda ambayo inafuatilia kila mtu wao katika ukoo wao, wakipangilia uharibifu utokee lini kwa mtu mmoja katika ukoo.

Mwishoni mwaka jana, dada mmoja kanisani kwetu akaniambia mara tu baada ya sikukuu ya Krismasi, familia za ukoo wao zitakutana kijijini kwa kusanyiko la kawaida kila mwisho wa mwaka. Nikamuuliza hata baada ya kuokoka bado unashiriki makusanyiko hayo ambayo ni maagano ya ukoo yaliyowekwa na mababu?

Akaniambia si hivyo. Nikasema, hakuna, ukishaokoka hupaswi tena kujumuika katika vikao vya aina hiyo kwani bado yapo mambo hufanywa kwa siri na wale wazee waliobakia kwenye ukoo. Kwa mfano lazima wanapochinja wanyama kama ng'ombe au mbuzi yapo maneno hutamkwa kuwataja mababu.

Hivyo, unapokula hicho chakula unaunganishwa na kilichotamkwa. Nilipomuuliza kwani ni lazima aende wakati huo na siyo wakati mwingine? Akajibu ni lazima kwani ili hata mmoja asikose, yaliandaliwa mabasi maalum kwa walioko Dar ili kusafiri na wasiokuwa na nauli maeneo mengine walitumiwa nauli ili waende.

Dada huyu, kwa muda mrefu amekuwa akisaka kijana wa kumuoa bila mafanikio. Alifikia hatua anamhoga kijana fedha ili amkubali kuwa mchumba wake bila mafanikio. Anayemtambulisha kwa wazazi, humvisha pete mwingine huku akitazama kwa macho yake, anabaki akishangaa. Ndipo nikawaza, kama bado ameunganishwa kwenye makusanyiko ya ukoo ilihali ameshaokoka kwa kumkiri Bwana kuwa ndiye mwokozi wake, yamkini ndio maana hatoboi katika eneo hilo.

Hata kama una elimu gani, mizimu haiangalii hilo, uwe mwana sayansi, mfanyabiashara mashuhuri, mwanajeshi, uwe umetembea dunia nzima, wote hawa ni wahanga wa nguvu za mizimu.

Kama hutashughulikia roho hizi za mizimu, hutaweza kupata amani katika maisha yako. Mizimu itaendelea kukufuatilia ili kuharibu maisha yako! Watu wengi leo walitakiwa kuacha kila kitu na kuchukua likizo kwa wiki kadhaa wafunguliwe kutoka katika roho hizi.

***Bila shaka msomaji wangu umejifunza kitu hapo. Wiki ijayo nitachambua zaidi baadhi ya dalili za mtu anayefuatiliwa na mizimu. Una kisa? Tuma ujumbe 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Mwaka 2023 uibue mikakati kutunza mazingira, kuvuna maji ya mvua

MWAKA 2022 umekwisha na leo tuko siku ya nane ya mwaka 2023. Yako matatizo tuliyovuka nayo na yako tuliyofanikiwa kuyamaliza ndani ya wakati husika.

Kwa uchache ambayo ni endelevu ni uharibifu wa mazingira uliochangia madhara mengi kama kutokuwa na mvua za uhakika, baridi kali, joto kali na majanga makubwa ya mafuriko, kimbunga na mengine ambayo yaligharimu maisha ya watu.

Kwa sasa sehemu kubwa ya ardhi imeharibiwa kwa udongo wenye rutuba kuzolewa kutokana na kilimo kisichozingatia kanuni za sekta. Pia kuna kuongezeka kwa kina cha bahari kiasi cha kumeza baadhi ya visiwa, ardhi ya kilimo na majisafi kwa binadamu na wanyama.

Ukame mkali umezikumba nchi zote na waathirika wakubwa ni Afrika ambako mifugo na wanyamapori wamekufa, binadamu wanahangaika kutembea umbali mrefu kutafuta huduma muhimu kama maji na chakula.

Kutokana na ukame, uhaba wa maji ulikuwa ni tatizo kubwa kiasi cha Dar es Salaam kuingia kwenye mgawo mkali, hali iliyoongeza gharama za maisha maradufu.

Pia kutokana na kupungua kwa kina cha maji kwenye mabwawa mengi ya kuzalishia umeme, mgawo mkali ulianza hali iliyoathiri shughuli za uzalishaji na maisha kuendelea kuwa magumu.

Vipindi vya mvua vimebadilika kiasi kwamba ni ngumu mkulima kuendelea kufuata ratiba ya kilimo kama ilivyokuwa awali, badala yake mavuno yamekuwa kidogo na kupaisha bei ya vyakula kila mahali.

Wakati hali hiyo ikiendelea lilikuja janga la UVIKO-19 ambalo licha ya kutangazwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kuwa limekwisha bado limeendelea kusumbua baadhi ya maeneo hata nchini.

Wakati linatangazwa kwisha lilishasababisha madhara makubwa kwenye uchumi. Kuna ambao maisha yaliharibika kabisa na kurudi kwenye umaskini, uchumi wa nchi ikiwamo Tanzania ulitikisika.

Wakati hilo likionekana kwisha ikatokea Vita ya Russia na Ukraine ambayo inaendelea hadi sasa, nchi ambazo zinaraslimali na bidhaa muhimu kwa ustawi wa watu.

Mathalani Ukraine ni mzalishaji mzuri wa ngano na mafuta ya alizeti asilimia kubwa ya nchi za Afrika zilitegemea bidhaa hizo kutoka huko, kutokana na vita bei imepaa mara mbili.

Russia ni mzalishaji wa gesi na mafuta. Kutokana na vikwazo vingi alivyowekewa na nchi za magharibi imekuwa ngumu kusafirisha bidhaa hiyo na sasa nchi hizo zinalazimika kutafuta kwingine na gharama kuongezeka maradufu.

Haya ni makubwa ambayo yanaendelea kuigharimu dunia,maisha ya watu na ustawi wao kwa sababu yanagusa nyanja zote za maisha.

Tunapoanza mwaka 2023 lazima mikakati endelevu iwepo katika kulinda na kutunza mazingira yetu ili tusiangamie sote. Inawezekana kabisa kupanda miti kwa wingi ili kurejesha uoto wa asili.

Wananchi wafundishwe namna rahisi ya kuvuna maji ya mvua ili yatumike nyakati za shida kwa kutumia matangi inawezekana kuhifadhi maji kwa kuyafanyia ukarabati mzuri ili yadumu muda mrefu na kuwa safi na salama.

**"Ukame mkali umezikumba nchi zote na waathirika wakubwa ni Afrika ambako mifugo na wanyamapori wamekufa, binadamu wanahangaika kutembea umbali mrefu kutafuta huduma muhimu kama maji na chakula.**

Kipindi kigumu tulichopitia kiliwaumiza wengi ilifika wakati watu walianza kutumia maji ya dukani ambayo wengi wasingeweza kumudu, sasa kutokana na fundisho hilo serikali inaweza kuja na mango wa kusaidia wananchi kwa kuweka ruzuku kwenye baadhi ya vifaa vya kuhifadhia maji.

Au kuwezesha uchimbaji wa visima maeneo mbalimbali nchini ambavyo vitavuna maji ya mvua,ikiwa gharama ya kuchimba visina itakuwa nafuu wengi watafanikiwa kuwa navyo maana yake watakuwa na majibya kusaidia wakati wa ukame.

Nchi zilizoendelea kama Dubai wanatumia maji ya bahari yanaondolewa chumvi na kutumika,licha ya ukame mkali kwenye nchi hizo lakini hakuna siku wamekutana na mgawo wa maji,jambo ambalo tunapaswa kujifunza kwa kuwa tumejaliwa vyanzo vingi vya maji na mvua.

Ni muhimu kutambua kuwa iwapo kila mtu kwenye eneo lake hatafanya jitihada za kulinda mazingira kwa ajili ya kizazi cha sasa na kijacho,kuna hatari kubwa inatunyemelea ambayo haitatuacha salama.

# BIRTHDAY








FAMILIA ya Riyaz Khan wiki hii ilikuwa na furaha baada ya binti yao Tahzeeb Riyaz, kutImiza miaka 16 na kufanyiwa sherehe za aina yake City Mall, jijini Dar es Salaam.





MITINDO

# ANZA 2023 KWA MAKOTI



MWAKA 2023 umeanza kwa kasi, suala la mitindo ya mavazi limebaki kuwa jambo muhimu katika maisha ya kila siku.

Jukumu la nguo gani unapaswa kuvaa linabaki kuwa lako binafsi, lakini uchaguzi ni lazima kuwa na uelewa mpana ili kupata nguo bora na maridadi.

Kutokana na umuhimu wake, tutakuwa na mwendelezo wa namna ya matumizi sahihi ya vazi aina koti na kanuni zake pale unapovaa.

Kwa ujumla kabla ya kupata aina yoyote ya koti katika mawasilisho yake yoyote, ni muhimu kuzingatia mambo kadhaa. Kwanza ni mtindo wako wa mavazi ya jumla. Hapa ndipo ladha inachukua jukumu la msingi wakati wa kuchagua kati ya aina tofauti za koti.

Hivi sasa kuna aina anuwai ya koti za wanaume kwenye soko. Haitofautiani tu kwa sura, bali pia kwa mtindo. Zimeundwa kwa nyenzo tofauti, ambayo inafanya utafutaji wako uwe rahisi zaidi.

Pili rangi pia hutumika kulingana na mahitaji yako na ni jambo la kuzingatia mapema.

**KOTI LA KISASA**

Aina ya makoti ya kisasa zaidi kwa wanaume na inawafanya waonekane wazuri.

Vazi hili linachanganya vizuri na mitindo ya doa na rasmi. Hii inafanya kuwa vazi kamili la kuvaa na suruali yenye kupendeza na pia kutumia na jinzi ya kawaida.

**BLAZER**

Blazer kwa wanaume ni kitu cha kupendeza, kwa hiyo inaweza kutumika ikiwa utaenda kufanya kazi au kwenda matembezi nje na marafiki.

Kumbuka kuwa aina hii ya koti ina tofauti ambayo inaweza kuifanya uwe na mwonekano mzuri.

Makoti ya mbugani

Ni koti aina ya kanzu lakini mguso wake sio rasmi. Inaelekea kuwa bora na mtindo wa mijini. Kipengele kinachojulikana zaidi ni kofia yake, ambayo imeundwa na nywele.

Kawaida huwa inafungwa kwa zipu na ina mifuko mingi. Ni nzuri kuvaa wakati wa safari msimu wa baridi au kukukinga wakati wa safari ya usiku.



UREMBO

Na Mary Geofrey



# JIPODOE NYUMBANI

HAKUNA ulazima kila unapotaka kutoka kwenda kufurahia maisha, basi utumie gharama kubwa kwa ajili ya kwenda kujipodoa saluni.

Unaweza kupaka vipodozi vyako ukiwa nyumbani na tena ukaonekana mwenye mvuto sawa na kwenda saluni ambako mara nyingi kunakuwa na watu wengi.

Leo katika safu ya urembo tutaelekeza kwa kifupi vitu unavyotakiwa kuwa navyo nyumbani ili kukuwezesha kutumia wakati wowote unapohitaji.

Hakikisha unakuwa na poda ya foundation, brashi, mascara, wanja na rangi za midomo.

**JINSI YA KUPAKA**

Anza kwa kupaka poda ya foundation, kisha chukua brashi ya kupakia vipodozi na chana nyusi zako.

Baada ya kuchana na kuziweka sawa anza kupaka wanja wako vizuri hadi uwe vile unataka.

Chukua makeup poda paka tena usoni, kisha Chukua Lipgloss paka ili kuilainisha kwanza kabla ya kupaka rangi ya midomo.

Baada ya hapo chukua lipstick yenye rangi nzuri, inayoendana na nguo unayovaa au unayoona inafaa kulingana na unakoenda kisha paka mdomoni ili kuzifanya lips zako zipendeze.

Hapo utakuwa tayari kwa ajili ya kuvaa nguo zako na kuonekana umedamshi zaidi.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Mexican Sosi na chapati za maji

CHAKULA cha Mexican sosi ni mchanganyiko wa kuku au nyama unayoweza kupika kwa aina tofauti.

Viungo vya mapishi haya huleta ladha na harufu nzuri na kukufanya upate utamu na raha ya kujiramba na huu msosi.

**MAHITAJI**

Minofu ya kuku robo kilo, Indian curry, cube maggie, limao au ndimu, tangawizi, pilipili manga, pilipili hoho, kitunguu kikubwa kimoja, mafuta ya kupikia na chapati za maji.

Namna ya kuandaa

Anza kuandaa nyama, ikate vipande vidogo na vyembamba sana ili iwe rahisi kuiva.

Osha na kisha nyunyuzia limao, weka chumvi, tangawizi na kitunguu saumu.

Changanya mchanganyiko, acha ikae kwa dakika kama 15 ili viungo vipate kuingia vizuri.

Andaa pilipili hoho, kitunguu maji na karoti, osha kisha kata kwa urefu, upate vipande virefu ambavyo vitapendeza kuchanganya kwenye nyama.

Bandika kikaangio au sufuria jikoni na weka mafuta ya kula ya kutosha. Acha yapate moto vizuri.

Weka nyama ya kuku, koroga kiasi na kisha acha ikaangike vizuri na subiria hadi nyama ipate kubadilika rangi na kuwa ya kahawia.

Weka mboga za majani, pilipili hoho, kitunguu na karoti. Funika kwa muda ili vipate kuiva na mvuke.

Weka kari kiasi, kisha koroga. Ni vizuri kama nyama itaanza kuwa na rangi ya curry.

Weka tangawizi kiasi, koroga na acha kwa dakika moja, weka pilipili manga ya unga, na kisha koroga vizuri.

Changanya 'Cube maggie' na kisha koroga, acha mchanganyiko kwa muda wa dakika tatu hadi tano ili uive vizuri. Kisha ipua chakula.

Andaa chapati zako na kisha weka nyama juu yake. Hapa chakula kinakuwa tayari kuliwa.



## MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Zingatia mambo haya wakati wa kupanga nyumba ya kuishi

MSIMU wa kutafuta nyumba za kuishi umewadia. Ni kipindi ambacho watu wengi ambao hawajabarikiwa kujenga, wanatafuta nyumba za kuhamia baada ya kumalizika kwa mikataba ile ya nyumba walizokuwa wakiishi.

Si kwamba wamechoka kuishi katika nyumba hizo, la hasha, bali baadhi wanataka tu kubadilisha mazingira.

Ni vyema katika kipindi hiki kuwa makini zaidi katika kutafuta nyumba ambayo haitakuletea shida. Kwa maneno mengine, hakikisha hukurupuki. Hakikisha unazingatia mambo muhimu kabla ya kufikia uamuzi wa mwisho wa kupanga nyumba kwa ajili ya kuishi.

Moja ya mambo ya kuangalia ni mahali nyumba ilipo na umbali. Kumbuka kuna uwezekano mkubwa ukaona nyumba nzuri kwa mwonekano na ukatamani upange kwa ajili ya kuishi, lakini ikawa iko mbali zaidi au ikakulazimu kutumia pesa zaidi kwa upande wa usafiri.

Endapo unatumia usafiri wa umma, itakulazimu kila ukifika kituoni ni lazima utumie tena usafiri mwingine ambao nao ni gharama kubwa kufika kwenye nyumba hiyo, hivyo ni lazima ufikirie kwa makini kufikia uamuzi wa kuishi kwenye nyumba hiyo la sivyo unaweza ukashindwa kuweka akiba kwa ajili ya kufanyia maendeleo mengine.

Jambo lingine la muhimu la kuangalia kabla ya kupanga nyumba ni kuangalia kama nyumba hiyo itahitaji marekebisho makubwa.

Kuna baadhi ya nyumba zinaonekana vizuri kwa nje, lakini ndani zinakuwa zinahitaji marekebisho makubwa ambayo huenda yakakuongezea gharama kubwa ambazo hukutegemea. Kwa hiyo inabidi ujiulize kama kuna ulazima wa kuishi kwenye nyumba hiyo au kama unaweza kutafuta nyingine na ukaepuka hayo isipokuwa tu kama mmiliki yuko tayari kurekebisha kwa gharama zake.



Jingine ni masharti yanayokuwa yamewekwa kwenye nyumba husika. Kwamba, baadhi ya wenye nyumba huweka masharti magumu na wakati mwingine mpangaji anapofika kuhitaji nyumba hawasemi ukweli na badala yake baada ya kulipia na kuanza kuishi ndio huanza kuyasema kidogokidogo kwa wapangaji, kwa hiyo ni vema kudodosa hilo kabla ya kufikia uamuzi wowote.

Hakikisha unausoma kwa makini mkataba kabla ya kulipa pesa yako kwenye nyumba. Wengi hufikiri ukishalipa kodi basi hakuna jambo la kwenda vibaya, lakini mambo yanaweza kubadilika.

Kama ambavyo unakubali kwa kuandika kwamba utalipa kodi kwa wakati na kuitunza vyema, hakikisha pia na mkataba wako unausoma vizuri na kama kuna mambo ambayo mwenye nyumba anapaswa kuyatekeleza, afanye hivyo. Kama ilivyo kwako na kama utabaini kama kuna kitu kinakufunga ni bora uulize mapema kabla ya kuingia rasmi kwenye nyumba.

Pia huu ni msimu wa mvua, hakikisha unazingatia endapo eneo la nyumba ilipo hapajai maji kwa sababu hilo nalo ni tatizo jingine linaloweza kukuletea shida..

## Njia za kupendezesha meza ya chakula



NDANI ya nyumba kuna aina nyingi ya meza, lakini meza ya chakula ndio ina changamoto kubwa katika kuipendezesha.

Hii ni kwa sababu ya umuhimu wake kwenye nyumba lakini wakati huo huo ikitumika kulia chakula.

Zifuatazo ni dondoo kadhaa za kupendezesha meza ya chakula bila kubughudhi kazi yake kuu.


1: Vyema kufahamu kuwa kuna maumbo matatu yaliyozoeleka zaidi ya meza za chakula. Maumbo hayo ni meza za pembe nne, za yai au za umbo la duara.

2: Weka vesi tatu, tepe tatu au mabakuli matatu yaliyowekwa maua au matunda yawe ni makavu au hai yakisambazwa katikati ya meza.

3; Weka trei katikati ya meza. Trei hiyo unaweza ukalibebesha vitu vidogodogo kama vile kichupa cha kuhifadhia chumvi ya mezani, vijiti vya kuondoa nyama katikati ya meno.

4: Weka mishumaa miwili pamoja na stendi yake kwenye kila upande wa meza.

# KATUNI




*KINYUNYIZO CHA LEO... ...HATA UKIDUNDIKA TUNAKUJUA UKWENI HAWAKUTAKI

# Watu 29 wauawa kwenye ghasia Mexico

**MEXICO CITY,** MEXICO

WATU 29 wameuawa wakati wa operesheni ya umwagaji damu ya kumkamata mtoto wa muuza dawa za kulevya maarufu nchini Mexico, anayefahamika kwa jina la "El Chapo.

Serikali ya nchi hiyo ilisema ilimkamata Ovidio Guzmán-Lopez, 32, anayedaiwa kuwa kiongozi wa genge la zamani la baba yake,linalojishughulisha na dawa za kulevya.

Alikamatwa Alhamisi huko Culiacan na kusafirishwa hadi jiji la Mexico City.

Kukamatwa kwake kulizusha ghasia na kusababisha askari 10 na washukiwa 19 kuuawa.

Wanachama wa genge lake wenye hasira waliweka vizuizi barabarani, walichoma moto makumi ya magari na kushambulia ndege katika uwanja wa ndege wa eneo hilo.

"Wanajeshi wengine 35 walijeruhiwa na watu 21 wenye silaha walikamatwa," alisema Waziri wa Ulinzi, Luis Cresencio Sandoval.

Guzman-Lopez, anayeitwa jina la utani "Panya" - alipakizwa kwenye helikopta na kusafirishwa hadi mji mkuu kabla ya kupelekwa katika gereza la shirikisho lenye ulinzi mkali.

Anatuhumiwa kwa kuongoza kundi la baba yake maarufu la Sinaloa, mojawapo ya magenge makubwa zaidi ya ulanguzi wa dawa za kulevya duniani.

Baba yake, Joaquin "El Chapo" Guzman, anatumikia kifungo cha maisha jela nchini Marekani baada ya kupatikana na hatia mwaka wa 2019 ya ulanguzi wa dawa za kulevya na utakatishaji fedha.

**BBC**




Lori lililotelekezwa likiungua moto barabarani baada ya wafuasi wa mtoto wa El Chapo kuzusha ghasia kupinga kukamatwa kwake na polisi wa Mexico juzi. **PICHA: DW**

# Mtoto amjeruhi mwalimu kwa risasi

**WASHINGTON,** MAREKANI

MTOTO mdogo wa kiume mwenye umri wa miaka sita anashikiliwa na polisi baada ya kumpiga risasi mwalimu wake huko Virginia nchini Marekani.

Mkuu wa polisi wa eneo hilo, Steve Drew, alisema tukio hilo limetokea katika Shule ya Msingi ya Richneck, katika jiji la Newport News.

Haijulikani ni jinsi gani mtoto huyo aliipata bunduki hiyo, lakini Drew alisema kuwa tukio hilo halikuwa la bahati mbaya.

Mwalimu huyo ambaye hakutajwa jina na anasemekana kuwa na umri wa miaka 30, amepata majeraha makubwa ya kutishia maisha yake.

Alipelekwa katika hospitali ya eneo hilo na anafuatiliwa kwa karibu na madaktari.

Tukio hilo lilitokea katika chumba cha darasa la kwanza chenye wanafunzi wa umri wa miaka sita hadi saba baada ya kutokea ugomvi kati ya wawili hao.

Lakini Drew alisisitiza kwamba ufyatuaji risasi huo umekuwa tukio la pekee na akasisitiza kwamba maofisa hawakuwa na taarifa kwamba kuna mtu alikuwa akizunguka maeneo ya shule akiwa na bunduki.

Maofisa walisema shule hiyo ina wanafunzi wapatao 550 ilikuwa na vifaa vya kugundua chuma ikiwemo silaha, wanafunzi walikaguliwa bila mpangilio na sio kila mtoto alikaguliwa.

Polisi walikataa kutaja silaha iliyotumika katika tukio hilo, lakini walisema kijana huyo alitumia bunduki.

Ofisa anayesimamia Shule katika eneo hilo, Dk. George Parker alisema maofisa watakuwa wakichunguza tukio lolote ambalo linaweza kuwa limesababisha tukio hilo.

"Tunataka kuhakikisha hakuna kitu kama hiki kinatokea tena."alisema.

Shule hiyo itafungwa Jumatatu, na kuahidi kuwa wanafunzi na wazazi watapewa msaada ili kuwasaidia kukabiliana na tukio hilo lililosababisha taharuki.

**BBC**

# McCarthy achaguliwa spika mpya Marekani

**WASHINGTON,** MAREKANI

KEVIN McCarthy amechaguliwa kuwa Spika mpya wa Baraza la Wawakilishi la Marekani, huku uchaguzi huo ukitawaliwa na majibizano makali ambayo karibu yashuhudiwe wawakilishi wa chama chake cha Republican washikane mashati.

McCarthy hatimaye alishinda nafasi hiyo baada ya duru 15 za upigaji kura, licha ya chama chake kuwa na kura nyingi katika bunge.

Ushindi wake umekuja baada ya kampeni kali ya shinikizo iliyofanywa na kushuhudiwa mubashara huku mmoja wa waasi wa chama Matt Gaetz, aliyekuwa hamuungi mkono mwanasiasa huyo alihimizwa kumpigia kura McCarthy.

Congressman wa Florida alikuwa miongoni mwa watu sita ambao walijiuzulu Ijumaa.

Hapo awali, huku kukiwa na majibizano makali, Gaetz alikuwa karibu apigwe na mwakilishi Mike Rogers, mfuasi wa McCarthy. Mbunge huyo wa Alabama alilazimika kuzuiwa na wenzake alipokuwa akimfokea na kumnyooshea kidole Gaetz.

Nchini Marekani Spika wa bunge hilo huweka ajenda za Bunge na husimamia shughuli za kutunga sheria.

Nafasi hiyo ni ya pili kwa ukubwa nchini Marekani kama ilivyo kwa makamu wa rais baada ya Rais wa Marekani.

**BBC**

# Mali yawasamehe wanajeshi 49 wa Ivory Coast iliyowakamata

**BAMAKO,** MALI

KIONGOZI wa kijeshi wa Mali, Kanali, Assimi Goita amewasamehe wanajeshi 49 wa Ivory Coast ambao walikamatwa mwezi Julai na kushtakiwa kwa kula njama dhidi ya serikali hiyo na kuibua mzozo mkali wa kidiplomasia.

Msemaji wa serikali, Kanali Abdoulaye Maiga, ambaye pia ni waziri wa utawala wa maeneo na ugatuzi ametoa tangazo hilo wiki moja tu baada ya mahakama kuwahukumu.

Watatu miongoni mwao walihukumiwa adhabu ya kifo bila ya kuwepo na 46 walihukumiwa adhabu ya kifungo cha miaka 20 jela kwa madai ya kujaribu kuhujumu usalama wa nchi.

Wanajeshi wa Mali waliwataja wanajeshi hao waliowasili katika uwanja wa ndege wa Bamako Julai 10, kama mamluki.

Ivory Coast na Umoja wa Mataifa walisema wanajeshi hao walisafirishwa kwa ndege ili kutoa ulinzi wa kawaida kwa kikosi cha Ujerumani cha ujumbe wa kulinda amani wa Umoja wa Mataifa nchini Mali.

**DW**

# Mapigano yaendelea nchini Ukraine

**KYIV,** UKRAINE

VIKOSI vya Russia na Ukraine vilikabiliana kwa silaha nzito Ijumaa baada ya pande moja kusema imeanza usitishaji mapigano.

Hata hivyo Ukraine ilipinga vikali kauli hiyo ya Russia na serikali ilisema kauli hiyo sawa na mtego.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Anthony Blinken, alisema nchi yake itatoa zaidi ya dola bilioni 3.75 ya msaada wa kijeshi kwa Ukraine na nchi zilizoathirika na uvamizi wa Russia.

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelenskiy, alisema wanachohitaji zaidi ni ahadi ya Marekani ya kuwasambazia magari ya kivita ya Bradley ili kukabiliana na Russia.

Makamu wa Kansela wa Ujerumani, Robert Habeck alisema Ujerumani inataka kutoa takriban magari 40 ya kivita ya Marder infantry kwa Ukraine kabla ya mwisho wa mwezi na kwamba inaweza pia kutuma silaha zake zote zinazofanya kazi.

**BBC**


**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF LANDS, HOUSING AND HUMAN SETTLEMENT DEVELOPMENT**
**REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT, (CAP 117)**

**CHANGE OF NAME DEED POLL**



BY THIS DEED, I IMANI MUSA ABDALLAH of P. O . Box 65 KILOSA MOROGORO, DO HEREBY wholly absolutly and utterly renounce, relinguish and abandon the use of my former name of KHADIJA M. ABDALLAH and adopt as from the date of this poll and in substitution of my formes name the name of IMANI MUSA ABDALLAH.

For the purpose of evidence of such determination I hereby declare that I shall at all times hereafter in all records, deedsdocuments and other writings and in all actions, suits and proceedings as well as in all public and private dealings and transactions and occations whatsover use and subscribe the said name of IMANI MUSA ABDALLAH

I hereby expressly authorize and require all and every person and whosoever at all times after the date hereof to designate, describe and adress me by the name of IMANI MUSA ABDALLAH

IN WITNESS WHEREOF I herein substitute my ald name of KHADIJA M. ABDALLAH by the nwe name of IMANI MUSA ABDALLAH and have set my hand ata Kilosa - Morogoro this 19th day of December 2022.

DEPONENT

This declaration has been subscribed before me this 19th day of December, 2022

COMMISSION FOR OATHS



**FOMU YA MIRATHI-2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo BOMA**
**Wilaya ya MOROGORO**
**Mkoa wa MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 03/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHENU HUSEIN SAID WA KIHONDA MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA MKUDE HUSEIN**

**TANGAZO**

(Kanunu ya 5 (2) kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 11 / Mwezi 01 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia;

Endapo kuna yeyeto mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

* Wosia wa Marehemu huyu upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika

**Imetolewa leo tarehe 06 mwezi 01mwaka 2023**

HAKIMU

# SAFU

## MAKALA

# KUPATA ELIMU NI JAMBO MOJA, KUELIMIKA NI JAMBO LINGINE



Na Magabilo Masambu

KUPATA elimu ni jambo la msingi na la lazima sana katika maisha ya kila mwanadamu, hasa katika maendeleo ya mtu na mtu, taifa na dunia kiujumla. Kutokana na umuhimu wa dhana hii, elimu inahitajika kwa kiasi kikubwa katika kuchochea maendeleo ya nyanja zote za kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Katika taifa letu, vijana wengi au makundi mengi ya watu, wamepata elimu ya kutosha lakini yawezekana kuelimika bado limekuwa tatizo kubwa kwa vijana hawa au makundi haya ya watu. Hii ni kwa sababu kupata elimu na kuelimika ni mambo mawili tofauti ambayo jamii inabidi ianze kutambua.

Ni dhahiri kuwa kibinadamu na kiutu, mtu asiye na kazi lazima naye ale chakula. Hawezi kubaguliwa kutokana na mila na desturi zetu. Kwa mantiki hiyo, kuna uwezekano mkubwa wa kurudi nyuma kimaendeleo katika eneo la uchumi wa watu wanaowahudumia vijana hawa wasomi wasio na kazi.

Matokeo ya kushuka kwa uchumi wa mtu mmoja mmoja yanasababisha kushuka kwa uchumi wa taifa kwa ujumla. Hii inatokana na ukweli kwamba vijana wengi hawatakuwa na kazi za kufanya na hiyo ni kwa sababu ya tafsiri mbovu ya uelewa juu ya kusudi la elimu na matumizi yake.

Wazazi na jamii wanapowapeleka watoto wao shule wanawakaririsha kazi za ofisini tu, hivyo mtoto anakuwa anajua moja kwa moja akimaliza masomo yake, atapata ajira serikalini au sekta binafsi. Hali hiyo inawafanya kushindwa kuwaza juu ya kutumia elimu yao katika vipaji au shughuli zingine muhimu zaidi. Hili pia ni tatizo linalofifisha ndoto muhimu za vijana wetu, wakiamini bila kuajiriwa hakuna maisha tena.

Watu wengi walipoingia kwenye ajira, waliamua kuacha ajira hizo na kuanza kupambania ndoto zao kwa kutumia elimu zao na kuleta matokeo makubwa duniani. Mfano, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Dk. John Pombe Magufuli, Robert Mugabe na wengine wengi, waliacha kazi ya ualimu na kupambania ndoto zao kupitia matumizi bora ya elimu walioipata na leo wameacha alama kubwa duniani.

Kwa maana hiyo, kupata elimu na kuelimika vyote vimetawaliwa na nguvu ya fikra na uamuzi. Ili mtu aelimike, anapaswa afanye uamuzi wa kutumia elimu yake katika maisha halisia kwa kuyatumia mazingira yake yanayomzunguka, ili kuimarisha maisha yake na maisha ya wengine pia. Vijana wengi sana baada ya kuwa wamepata elimu, wamekuwa wakijua tayari wameshaelimika kwa sababu wanavyo vyeti tayari kumbe elimu ili ilete faida ni lazima watu waitumie katika maisha yao ya kila siku.

Kusudi kuu la elimu, ni kupata maarifa yanayoifanya akili iyambulike kwa urahisi zaidi, juu ya kutenda shughuli mbalimbali ambazo mhusika anahitaji kufanya katika maisha yake. Mfano mtoto wa kike anapopata elimu kuhusu mapishi, inakuwa rahisi sana kwake kuendesha shughuli za mapishi na kumfanya afikie malengo yake kwa urahisi zaidi.

Ni ukweli kwamba katika nchi yetu kuna baadhi ya vijana wasomi, wako wachache walioamua kuelimika na kwa sasa wameamua kuiwekeza elimu yao katika mambo ya kiuchumi, kuendesha maisha yao na kuzalisha ajira kwa Watanzania wengine. Baadhi wamejikita katika kilimo cha kisasa na viwanda vidogo vidogo vya usindikaji kupitia mikopo na ruzuku mbalimbali kutoka serikalini. Hao tunawapongeza kwa dhati kabisa.

Lakini wakati vijana hao wachache walioamua kuitumia elimu kuendesha miradi yao mbalimbali, baadhi ya vijana wanaojiita wasomi wenye elimu bila matumizi, wamejikita kudharau shughuli za kujiajiri katika kilimo na baadhi ya kazi za kimaendeleo. Leo hii wako ambao wamekataa hata kuongea lugha za makabila yao, kwamba ni kujiaibisha!

Wengine hata wanapokuwa wanasubiri matokeo yao ili kuendelea na masomo, huona vigumu hata kwenda mashambani kusaidia wazazi wao. Hilo ni jibu tosha kuwa vijana wengi wako katika ulimbukeni kuwa elimu ni kuja kuajiriwa ofisini, jambo ambalo si kusudi kuu la elimu.

Serikali ianzishe mpango mkakati na imara katika kuwasaidia vijana kwa kuwatengenezea mazingira mazuri katika kuanzisha, kuendeleza na kukuza vipaji na miradi yao baada ya kuhitimu masomo yao. Mazingira hayo ni pamoja na kuweka kipaumbele katika wizara ambazo zinaweza kutengeneza vijana wengi kujiajiri. Mfano kilimo cha kisasa, ufugaji wa kisasa, usindikaji kupitia viwanda vidogo vidogo na kuwarahisishia mifumo ya usajili masoko na mitaji kupitia ruzuku na mikopo ya serikali na mabenki binafsi nchini.

Ikiwa serikali inaendelea na mchakato wa kuielimisha jamii kama nilivyoshauri juu ya kusudi kuu la elimu na umuhimu wake katika maisha yetu, inabidi pia iendelee kufanya tathmini juu ya aina hii ya elimu iliyopo nchini ili kujua kama ni rafiki kwa vijana wetu kuitumia katika mazingira yetu au la. Ni lazima tuanze kubadili mfumo huu uliopo kuhofia kuangamiza vijana wetu.

Kushindwak ufanya hivyo, itakuwa hasara kubwa kwa taifa kupitia kutumia pesa nyingi za watanzania walipakodi, kutoa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu kwa ajili ya kupata elimu ambayo inaweza isiwasaidie na kushindwa kuzirudisha kwa ajili ya maendeleo mengine ya umma na kufanya nguvu inayowekezwa kwa wanafunzi hawa kutoleta matunda badala yake, kutengeneza kundi la vijana tegemezi na kuifanya taasisi ya elimu kuongoza kwa kutengeneza maskini bora na ombaomba wa misaada zaidi kutoka mataifa ya kinyonyaji yaliyoendelea jambo ambalo litapelekea kuumizaa nchi yetu.

Vijana ni nguvu kazi chanya kwa taifa letu endapo tu wakiandaliwa mazingira bora. Kinyume na hapo, vijana hawa wanaweza kuwa nguvu kazi hasi kwa taifa ikiwa serikali haijawaandalia mazingira bora, nguvu ambayo inaweza kurudisha taifa nyuma kwa kasi kubwa na kuangamiza kizazi na kizazi cha watanzania wengi.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**DAR ES SALAAM-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Wimbo 'Nimwokoe Nani' wa NUTA ulivyoacha swali lililokosa majibu sahihi zaidi ya miaka 50*



Na Adam Fungamwango

NI zaidi ya miaka 50 sasa imepita tangu bendi ya NUTA Jazz iliporekodi kibao kilichowashangaza wengi kinaitwa 'Nimwokoe Nani.'

Kibao hicho kilitungwa na mwanamuziki nguli nchini, Muhidini Mwalimu Gurumo, ambaye ni mmoja wa waanzilishi wa bendi hiyo. Lakini mbali na kuwa mwaka 1978 aliihama bendi hiyo wakati huo sasa ikiitwa JUWATA Jazz, akahamia Orchestra Mlimani Park, mwaka 1985 akaenda bendi ya Orchestra Safari Sound. Alirejea tena kwenye bendi yake hiyo ya awali ambapo ilikuwa tena imeshabadilishwa tena na kuitwa OTTU Jazz hadi alipofariki dunia 2014.

Wengi walishangazwa na aina hiyo ya utunzi, ambao ulikuwa na swali tata na lenye kuleta mkanganyiko mkubwa kwenye jamii.

Wimbo huo ulikuwa ni kama chemsha bongo, au mtihani. Uzuri wake kila mmoja alitakiwa kujibu anavyoona yeye, lakini kila anayejibu kwa maoni yake mjadala mkubwa unazuka.

Wimbo huu uliorekodiwa mwaka 1970 uliondokea kuwa wimbo maarufu sana, ukapendwa na mashabiki wengi wa muziki kutokana na maneno, mpangilio wa sauti na mirindimo, lakini linapokuja suala la maudhui, inakuwa ni changamoto kidogo.

Watu wanapokaa kwenye vijiwe na sehemu mbalimbali ambazo wanazungumzia muziki, ubishi unakuwa mkubwa sana.

Hebu kwanza kuangalia mashairi ya wimbo huu 'Nimuokoe Nani', halafu ndiyo tunajua ni kwa nini watu walikuwa wanabishana sana.

Kwa ufupi tu ni kwamba kulikuwa na mtu mmoja na familia yake, akiwa na baba na mama yake, mkewe na mtoto mmoja. Walikuwa wanasafiri majini kwa kutumia ngalawa, lakini ilipofika katikati ya bahari, ilizama.

Sasa ikawa ni kama jamaa anawapigia watu simu au kuwasiliana na watu waliokuwa nchi kavu kuwa yeye ana uwezo wa kuogelea mwenyewe, pia kumuokoa mtu mmoja tu. Hawezi kuokoa wawili kwa sababu atashindwa kuogelea. Uwezo wake ni wa mtu mmoja. Sasa kati ya hao amuokoe nani.

"Ndugu zangu nauliza leo ili nipate kufanikiwa, nilikuwa mimi na baba, mama mke na mwanangu, tulifanya safari tukiwa ndani ya ngalawa, katikati ya bahari, ngalawa yetu ilizama.

Ndugu zangu nifahamisheni, nimuokoe nani? Wa kwanza baba wa pili mama, wote wakinitegemea, mke wangu na mwanangu wote wakinitegemea, uwezo wangu ni wa mtu mmoja sasa nifanye nini?" Shughuli ipo hapa.

Wimbo huo ulipotoka kila mmoja alikuwa na mtazamo wake. Hata leo hii kila mtu atakuwa na mtazamo wake. Kila mmoja anamuuliza mwenzake,"wewe kama ikitokea hivyo utamuokoa nani?"

Wengine wanajibu kinafki. Anaweza kumtaja mmoja wapo mbele za watu lakini moyoni wake anaye ambaye kama ikitokea atamuokoa.

Na hapo ukiangalia sana yoyote ambaye mtu atasema ndiye atakayemuokoa, basi ndiyo anayempenda sana kuliko wengine.

Watu wamebishana sana. Wapo waliosema wao watamuokoa mtoto kwa sababu bado ana umri mdogo kuliko wengine ambao umri wao umekwenda. Wapingaji wanawajibu kuwa mtoto atazaliwa mwingine, hatakiwi kuokolewa hapo. Wengine wanatisha kuwa unaweza kumuokoa mtoto halafu kubwa hakuwa wako halali, alikuwa na baba yake kwa sababu siri ya baba wa mtoto anaijua mama. Unaweza kukutana na jamaa akakwambia huyo ni mtoto wangu twende tukapime DNA.

Kuna wanaosema kama ikitokea basi wangemuokoa baba. Hao pia wanakutana na ukosoaji kuwa huwezi kumuokoa baba na kumuacha mama aliyekuweka tumboni miezi tisa, akakunyonyesha. Wakaenda mbali zaidi wakidai inawezekana hata huyo baba unayemuokoa akawa si halisi kwa sababu zile zile za siri ya baba wa mtoto anaijua mama. Unadhani baba yako, unamuokoa kumbe alisingiziwa, halafu ukawa umemwacha mama yako mzazi. Hakuna mama wa kusingiziwa duniani.

Wengine wakasema bora tu uokoe mke. Na jibu hili lilijibiwa hata na bendi ya JKT Kimbunga Stereo. John Simon alijibu swali hilo kwa rafiki yake Gurumo ambaye walikuwa naye NUTA Jazz wakati inaanzishwa lakini baadaye akatimkiia bendi hiyo.

"Kama ni mtoto utapata mwingine, baba na mama wamekula chumvi nyingi. Epukana na lawama ya kumuokoa mmoja kati ya wazazi wako ewe kaka. Muokoe mkeo utapata watoto ambao watakuwa sawa na wazazi wako." Haya ni baadhi tu ya mashairi yaliyokuwa kwenye wimbo wa 'Jibu Nimwokoe Nani.'

Wimbo ulikuwa mzuri mno, ulipangiliwa, mirindimo na sauti za waimbaji zilikuwa za viwanho vua hali ya juu. Wengine waliafiki. Lakini kama kawaida kwenye wimbo huu kila mtu ana mtazamo wake. Jamaa wakadaiwa kuwa unaweza ukamuokoa mke halafu baadaye mbele ya safari 'akakuzingua' au 'mkazinguana', mkaachana. Au akakutoroka. Hapo utaanza kujuta ni kwa nini siku ile sikumuokoa mmoja wapo kati ya wale waliokuwepo na si huyo.

Nimeliruidisha tena swali hili hapa, unaweza kunitumia meseji na kuaniambia kwa maoni yako unadhani nani kati ya hao mmoja tu ambaye angepaswa kuokolewa?

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Harusi imevunjika-13

HAKUNA aliyeamini alichokisikia, wala aliyeamini macho yake kwa kile alichokiona. Awali kulikuwa na vigelegele, ngoma, bashasha na furaha tele kwa watu wote waliohudhuria harusi hiyo. Bwana harusi Jerry Mohamed aliliongoza kundi la ndugu, rafiki na jamaa kutoka Dar es Salaam kwenda Kibaha kwa Mathias mkoani Pwani kwa ajili ya kufunga ndoa na mwanamke Vayajo waliyekubaliana kuoana. Mabasi, magari, bajaji, bodaboda, vyote vilimiminika kwenda huko kila mmoja akiwa na furaha tele. Kilichotokea ndicho kilicholeta mkasa mzima kwenye sakata hili la aina yake. Nini kimetokea? Kwa nini? Sababu ni nini? Na baada ya hapo nini kinaendelea? Kila nakala yako ya Nipashe itakupa majibu ya kisa hiki cha kushangaza.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

MMMH! Vayajo, umekataa vipi wakati umemtoroka hapa mwenzako?"

"Wee Naa wee, nilikataa, ndiyo maana nilikubali hadi mipango yote ya harusi inafanyika, akawa ananiletea meseji hapa, yaani Vayajo kweli umekubali kuolewa na huyo mwanaume wakati mimi nakupenda. Nikamwambia mimi nafuata maisha, wewe huna kipato kikubwa hata cha kutunza mwanamke akaishi kwa raha. Akaniambia mwenzako sasa hivi nina mchongo, ukikubali hiyo nitakuwa milionea, nikamwambia haya tutaona. Dada we siku moja kabla ya ndoa, akanipigia simu akaniambia mambo yameshatiki nina pesa za kumwaga, nina mamilioni hapa sina hata wa kutumia naye, nakutaka wewe la azizi wangu, mwenzangu kusikia hivi nikapagawa."

"He, makubwa dada wewe ndiyo yalikuwa hayo eee."

"Shoga yangu nikamwambia hapa niko ndani, mimi bi harusi kesho naolewa. Akaniambia utajiharibia mwenyewe, mimi sasa hivi ni tajiri, nimeshapiga pesa maana na nataka niishi na wewe, lengo lipo pale pale. Nikamwambia kama unataka kuishi na mimi basi na niamini kama kweli una hizo pesa, weka shilingi milioni tano kwenye akaunti yangu.

Mama we, akaniomba namba za akaunti. Kwani ilifika hata robo saa, kwenye ujumbe wangu wa simu ikasoma nimeingiziwa shilingi milioni saba, sikuamini, nilipagawa. Sasa hapo nilikuwa niko tayari kufanya chochote shoga. Nilikuwa hapo tena na hiyo ndoa? Mimi napelekwa saluni hapo akili yangu haipo kabisa hapa."

"Mmmh! Shoga yangu una mambo weee."

"Mambo kidogo shoga, basi narudi akanipigia simu, nikamwambia mimi sasa hivi natembea na wapambe kwa hiyo asipige simu anaweza kuharibu dili, atume tu meseji, ndiyo akaniambia amempigia simu dada yangu Pude. Hivi unajua yeye peke yake ndiyo anajua kila kitu na yeye ndiye aliyefanya maarifa ya mimi kutoroka bila mtu kujua. Nyinyi mlikuwa mnamuona kwenye sherehe, kumbe yule kaka kampigia simu akamwambia kila kitu na yeye akapigwa laki zake tano. Pude akaja akaniuliza, nikamwambia dada mimi niko tayari kuondoka, sijali chochote kitakachotokea, pesa hizo siyo mchezo. Tukaanza kupanga mbinu sasa za kutoroka. Tutatorokaje na umati ule?"

Vayajo aliendelea kufichua mbinu alizotumia siku ile kutoroka kwenye harusi, akiwa yeye ndiye anasubiriwa kuolewa. Akatoroka katikati ya kundi la watu ambao walikuwa nje wakiserebuka kwa disco na ngoma mbalimbali.




**"Siyo hivyo Vayajo, maana naona unazunguka huku na huko, kweli nimeshajua jinsi ulivyoishi na alivyokuwa anakupenda, anakujali, sasa tatizo nini?"**

"Enhee lete ubuyu shoga." Nasma akachombeza.

"Pude alitoka sijui kaenda wapi, kurudi alikuwa ameficha mkongojo, sijui kaupata wapi, dada yangu yule naye mpana kama tambara la sinema. Ana mpunga wake kibindoni mama, utamtaka.

Kwa bahati nzuri wakati anaingia chumbani hakukuwa na mtu yoyote, akaniambia nitoke twende kwenye chumba kingine ili nijiendae kutoroka. Tukaingia chumba kingine. Nikavalishwa mama kama bibi kizee, nikaambiwa nishike na mkongojo. Shungi langu liko wapi dada, kichwani, nikaambiwa sasa utembee kama bi kizee, nakutoa hapa, halafu mbele nimeshakodisha bajaj, unapanda nakupeleka hadi Kibaha Kwa Mathias kituoni, mimi narudi huku kwenye sherehe maana nisije kuonekana nimekutorosha kama na mimi sitoonekana."

"Pu, huyo dada yako mkubwa nimemvulia kofia mwaya,"

"Yaani bila yeye hata nashangaa ningeondoka vipi kwenye umati ule, natoka pale nikajifanya kama bi kizee, nasikia watu tu bibi mbona unaondoka, babu kakupigia simu nini anauliza ugali, sikukohoa wala nini, ila kicheko kilikuwa kinanibana, nikatembea peke yangu na mkongojo, Pude akanifuata nyuma nyuma ili isionekana kama tuko safari moja, nikaikuta bajaj mbele, nikapanda na yeye akaja akapanda. Hapo bibi tukafanikiwa kutoroka."

"Mwe nyinyi mna hatari, sasa mngebambwa mngefanyaje?"

"Tungejua hapo hapo cha kujitetea, akili yetu yote ilikuwa huko."

"Haya mwaya, hebu niambie, ulipofika huko ikawaje?"

"Bibi wee, nilimkuta, nilimkuta ananisubiri kwa hamu. Nikamwambia haya baba, mwenzako nimetoroka kwenye harusi, nimeharibu kila kitu, kuanzia sherehe yenyewe mpaka heshima kwa wazazi wangu na kijiji kizima, unasemaje?

Aliponiona tu jinsi nilivyopambwa na piko, akajua kabisa ni kweli. Akasikitika kidogo, akaniomba radhi lakini akasema atanifuta machozi.

Kusema kweli nikaishi naye kwa raha sana. Alikuwa na pesa sikudanganyi, siku chache tu nilikuwa kama malaika, nikapelekwa sehemu zote za starehe, niseme nini mwanamke mimi nisinunuliwe, nikasema mwanaume si huyu, nilikuwa nataka kupoteza muda kwa Jerry tu. Hapo shilingi milioni zangu saba ziko benki zimetulia. Baadaye nikamdanganya kuwa nyumbani kuna shida sana mama anaumwa na amepelekwa hospitali, kumbe aliyepelekwa ni Zulfa, huku na huku nikapata shilingi milioni tatu, nikaziweka tena benki."

"Kweli bibi umevuna. Sasa imekuwaje umerudi tena huku? Mmegombana? Maana kwa raha hizo umerudia nini tena huku kijijini vumbi tupu, kama mimi ningemng'ang'ania, au na yeye ukamtibua, maana wewe..."

"Usiwe na haraka shoga yangu kama unaogea nje."

"Siyo hivyo Vayajo, maana naona unazunguka huku na huko, kweli nimeshajua jinsi ulivyoishi na alivyokuwa anakupenda, anakujali, sasa tatizo nini?"

"Makubwa we shoga yangu acha tu. Kwanza tayari nimeshakumaliza, angalia ulivyopendeza na hizo nywele zako."

Nasma akaangua kicheko cha kimbea. Akachukua kioo na kujitazama. Akaridhika na jinsi alivyojiona. Akatabasamu.

"James leo akinione, hawezi kuniruhusu kuzurura hapa kijijini."

"Na alivyokuwa na wivu shemeji yangu yule loh!"

"Enhee tuendeleee na mastori yetu."

"Basi dada, mwanaume alikuwa tayari keshakolea, na kaniambia atanioa.

Tukawa tunabishana, atapelekaje tena barua wakati kuna barua ilishajibiwa na harusi ikataka kufanyika, nikamwambia muolewaji ni mimi na bado ndoa ilikuwa haijapita kwa hiyo, nikamshusha presha kaka wa watu kuwa barua yake itapokelewa tu na hata isipopokelewa upande wa baba, ipelekwe hata upande wa mama kwa wajomba zangu, wanaweza kusimamia tu mchakato nikaolewa, basi tukakubaliana na Japiru wangu. Sasa shoga kilichotokea. Ndiyo hicho ambacho kimenifanya leo unione nimekuja tena kuishi huku. Ingekuja labda kutembea tu, lakini siyo kurudi moja kwa moja."

"Hapo ndiyo nilikuwa napataka mimi."

"Mmmh! Muangalie kwanza, yaani mpaka unakaa vizuri, maana unaona kama utakuwa husikii, Naa wewe kwa umbea, ile ole wako nisikie hizi habari zimevuja hapa kijijini."

ITAENDELEA JUMAPILI

# HARMONIZE ANABAKI AKIWEWESEKA AKIMUONA FEZA



NI majibu yenye ukweli lakini yamejaa utata ambayo CEO wa Konde Music Worldwide, Harmonize ameyatoa baada ya watu kujadili ukaribu wake na Feza Kessy.

Harmonize ameandika kupitia ukurasa wake wa Instagram, kwamba watu wanaposema yeye na Feza wamependeza wanajikuta wanachanganyikiwa, lakini wao wenyewe wanaona.

Feza amepamba video ya wimbo wa Harmonize 'Wote' na kufanya mambo adimu kutokana na jinsi alivyokuwa huru kiasi cha kuibua minong'ono kwamba wawili hao wapo katika uhusiano wa kimapenzi.



## P Funk Majani amkubali Gachi

MTAYARISHAJI mkongwe wa muziki wa BongoFleva nchini, P Funk Majani, amemtaja Gachi kuwa ndiye mtengeneza muziki bora kijana 2022.

Amesema Gachi amekuwa mahiri katika kazi zake za kuandaa muziki kwa umakini na ubora wa hali ya juu.

P Funk ameuambia mtandao wa Bongo5 kuwa Gachi ni mmoja kati ya watajarishaji wa audio za muziki ambao wameshiriki kwenye albamu ya kwanza ya TNC ambayo inawahusisha Temba , Juma Nature na Chege.

"Gachi ana njaa sana, wapo wengine akina Touch lakini huyu jamaa kwa vijana hawa anafanya mambo yake kwa ukubwa sana" amesema Majani.

HABARI MICHEZO

ZISIKUPITE

### DEPAY AITAMANI UNITED

MSHAMBULIAJI wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Memphis Depay mwenye umri wa miaka 28 anataka kujiunga tena na Manchester United ikiwa ni baada ya miaka sita kuondoka Old Trafford. (***Sport***)

### JUDE ATAKIWA CITY

KLABU ya Manchester City inapanga kuboresha safu yao ya kiungo msimu ujao kwa kumwongeza mchezaji wa kimataifa wa England anayekipiga Borussia Dortmund, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19. (***ESPN***)

### HATIMA YA BELLINGHAM

KLABU ya Borussia Dortmund inatarajia uthibitisho wa Jude Bellingham katika wiki zijazo kuhusu wapi anataka kucheza msimu ujao, huku Liverpool, Real Madrid na Manchester City zikisubiri kwa hamu uamuzi wake. (***90Min***)

### CHELSEA, SHAKTAR ZATETA

CHELSEA wanaendelea na mazungumzo na Shakhtar Donetsk kuhusu usajili wa winga wa Ukraine, Mykhailo Mudryk mwenye umri wa miaka 22 na kiungo wa kati wa Benfica wa Argentina, Enzo Fernandez (21), baada ya kukamilisha dili la kumsajili kiungo, Andrey Santos mwenye (18) kutoka Vasco da Gama ya Brazil. (***Metro***)

### ARSENAL YAMKATAA MUDRYK

ARSENAL haitaki kujiingiza katika vita na Chelsea ya kutaka kumnunua Mykhailo Mudryk huku wakiongeza nguvu mipango yao ya kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ureno, Joao Felix kutoka Atletico Madrid. (***Telegraph***)

### ARTETA AMTAKA JOAO

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta anashinikiza klabu hiyo kuwasajili Mykhailo Mudryk na Joao Felix katika dirisha la usajili la Januari ambalo linaelekea ukingoni. (Mirror)

### ABOUBAKAR ANUKIA UNITED

KLABU ya Manchester United imekubali kumsajili mshambuiaji wa Timu ya Taifa ya Cameroon, Vincent Aboubakar mwenye umri wa miaka 30 kwa mkataba wa mkopo kutoka Al Nassr ya Saudi Arabia. (***OKAZ, via Talksport***)

### JUVE, BARCA MAWINDONI

JUVENTUS na Barcelona zinafuatilia kwa karibu hali inavyoenda ya mkataba wa mshambuliaji wa Ivory Coast, Wilfried Zaha katika klabu ya Crystal Palace, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 anaingia katika miezi sita ya mwisho ya mkataba wake huko Selhurst Park. (***Evening Standard***)

### CAICEDO ATAJWA LIVERPOOL

LIVERPOOL na Chelsea wanaisaka saini ya kiungo wa kati wa Brighton na Timu ya Taifa ya Ecuador, Moises Caicedo ambaye ana umri wa miaka 21. (***Sky Sports***)

### THURAM ATAJWA CHELSEA

CHELSEA imeonyesha nia ya kumsajili mshambuliaji wa Borussia Monchengladbach, Marcus Thuram, mwenye umri wa miaka 26 katika dirisha dogo la usajili la mwezi huu. (***Foot Mercato***)

### MOYES MAMBO MAGUMU

KOCHA wa West Ham, David Moyes anakabiliwa na wiki mbili muhimu, huku mechi za Ligi Kuu England dhidi ya Wolves na Everton zikipangwa kuamua mustakabali wake. (***Mail***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# TEN HAG AFUNGUKA RASHFORD HAZUILIKI

## Afurahishwa na kiwango cha mshambuliaji huyo, Lampard naye asema...

**MANCHESTER,** England

KOCHA Erik ten Hag amesema Marcus Rashford "hawezi kuzuilika" baada ya mshambuliaji huyo wa Manchester United kufunga bao katika mechi tano mfululizo.

**Rashford alifunga mabao mawili na kufunga lingine kwa United iliyosonga mbele katika mashindano ya Kombe la FA kwa kupata ushindi wa magoli 3-1 dhidi ya Everton, mechi iliyochezwa Uwanja wa Old Trafford juzi.**

Ni mara ya kwanza kwa Rashford kufunga bao katika mechi tano mfululizo kwa United baada ya kufumania nyavu katika kila mechi tangu fainali za Kombe la Dunia kumalizika. "Marcus ndiye aliyetangulia na alionyesha kujiamini, na imani na harakati nzuri nyuma, akiwachukua wachezaji," alisema bosi wa United Ten Hag.

"Nadhani dakika 90 alikuwa tishio kwa sehemu ya ulinzi ya Everton.

"Ni juu ya kumleta katika nafasi sahihi hivyo Marcus anafanya vizuri sana lakini pia analeta nguvu zake na kutozuilika kwa kasi yake na chenga zake."

Kocha wa Everton, Frank Lampard, pia alitowa sifa tele kwa Rashford, akiongeza "hakuna anayeweza kumzuia".

Mshambuliaji huyo ameshafunga mabao 13 kwa msimu huu, tayari nane zaidi ya aliyofunga katika msimu mzima wa 2021-22.

"Kama mshambuliaji, unapima mabao na asisti na hakika leo (juzi), alikuwa na asisti mbili na bao moja," aliongeza Ten Hag.

"Ana ujuzi wa ajabu na anapokuwa na utulivu huo wa kiakili anaweza kuendelea, lakini hilo linadai mengi kutoka kwake na kwetu, lakini anapoweka umakini hivyo nina uhakika anaweza kuendeleza mchakato huu."

Ushindi dhidi ya Everton ulikuwa wa saba mfululizo kwa United katika mashindano yote.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
MANCHESTER CITY
VERSUS
CHELSEA
1 | 1.40
X | 4.51
2 | 6.81

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# DEMBELE HATAKI KUONDOKA BARCELONA



**BARCELONA,** Hispania

OUSMANE Dembele "anafuraha ndani ya Barcelona" na anataka kusalia, huku kukiwa na ripoti zinazomhusisha na kuhamia Paris Saint-Germain ya nchini kwao Ufaransa.

Dembele amekuwa na wakati mseto katika LaLiga tangu alipowasili Barca kwa fedha nyingi akitokea Borussia Dortmund mwaka 2017, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 amekuwa na msimu mzuri tangu Xavi achukue usukani msimu uliopita.


Amehusika katika mabao mengi kuliko mchezaji mwingine yeyote wa Blaugrana hao tangu Xavi alipokuwa kocha mkuu Novemba 2021, akifunga mabao nane na kutoa asisti 20.

Hiyo inajumuisha mabao sita na asisti saba katika mechi 22 msimu huu (michezo 17 ameanza), na Dembele pia alitoa pasi mbili za magoli katika michezo saba aliyoichezea Ufaransa walipomaliza kama washindi wa pili katika fainali za Kombe la Dunia zilizomalizika nchini Qatar.

Hata hivyo, licha ya stori zinazodai kuwa PSG wanaweza kumsajili kwenye Ligue 1, winga huyo wa zamani wa Rennes alikiambia kituo cha televisheni cha Eleven Sports cha Ubelgiji kwamba hataki kuondoka Camp Nou.

"Nilisaini mkataba mpya Barca miezi minne iliyopita na nina furaha hapa, nataka kuendelea kufanya kazi na kuimarika Barcelona," alisema.

Dembele amebakiza miezi 18 tu katika mkataba wake, lakini rais wa Barca Joan Laporta alisisitiza Alhamisi kwamba "hauzwi", akiambia Sport: "Ikiwa PSG watakuja kumsajili, tutawaambia hauzwi.



# Van Dijk aipa pigo Liverpool

**LIVERPOOL,** England

MLINZI wa Liverpool, Virgil van Dijk atakuwa nje ya uwanja kwa zaidi ya mwezi kutokana na jeraha la misuli ya paja huku akiuguza jeraha jipya, Kocha Jurgen Klopp, amesema.

Van Dijk alipata jeraha katika mechi ya Liverpool ilipofungwa mabao 3-1 na Brentford Jumatatu iliyopita na akatolewa wakati wa mapumziko.

"Lilikuwa pigo kubwa," alisema Klopp katika mkutano na wanahabari hapo juzi.

" Nilimtoa, haikuwa wazi labda angejaribu kucheza. Utambuzi ulikuwa mkali sana. Tunazungumza juu ya wiki, zaidi ya mwezi lakini natumaini atarudi mapema uwanjani.

"Kila kitu kiko sawa kwa timu lakini kwa Virgil ni vigumu kwake. Amecheza mechi nyingi ajabu kwa miaka mingi. Hatuwezi kumtumia uwanjani lakini nje ya uwanja tutafanya hivyo."

Wakati huo huo, Liverpool itafurahia kuongezwa kwa mchezaji mpya, Cody Gakpo, na Klopp alisema amefurahishwa na winga huyo katika siku zake za kwanza za mazoezi.

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# NKOMA AUTAMANI UBINGWA, YANGA PRINCESS IKIENDA CAF

**Na Shufaa Lyimo**

LICHA ya timu yake kupata ushindi mnono wa mabao 5-2 dhidi ya Alliance Girls katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam juzi, Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Sebastian Nkoma, amesema anahitaji kuendelea kukiboresha kikosi chake.



Sebastian Nkoma

Matokeo hayo yameifanya Yanga Princess kufikisha pointi saba na kupanda hadi katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa nyuma ya vinara, JKT Queens yenye pointi 10 na Fountain Gate Princess yenye pointi tisa wakati mabingwa watetezi, Simba Queens yenye pointi saba ikifuatia.

Nkoma alisema bado ana kazi ya kukijenga kikosi chake ili kiwe bora kwa ajili ya kukabiliana na ushindani uliopo kwenye ligi hiyo msimu huu.

"Ninashukuru tumepata pointi tatu katika mchezo huu ingawa kuna makosa ambayo bado ninaendelea kuyafanyia marekebisho ili kikosi changu kicheze soka la ushindani katika michezo iliyopo mbele yetu," alisema Nkoma.

Hata hivyo kocha huyo aliwapongeza wachezaji wake kwa juhudi walizozifanya katika mechi hiyo ambayo walipata ushindi mnono akiongeza ni matunda ya ushirikiano wa wachezaji wote wa timu hiyo.

"Wapinzani (Alliance Girls) wetu sio wabaya, timu yao ina wachezaji wachanga, walijitahidi kutushambulia isipokuwa bahati haikuwa kwao, malengo yangu ni kuchukua ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake msimu huu," alisema kocha huyo.

Aliongeza wamejipanga kucheza soka la ushindani na kuongeza nguvu katika kila idara ili watimize malengo ya kuivua Simba Queens ubingwa na kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa.

## Saa zahesabika hatima Fei Toto

INATOKA UK. 24

ga kwa muda wote waliokaa pamoja.

Inadaiwa ofa ambayo amepewa Fei Toto mwenye mabao sita katika Ligi Kuu Bara msimu huu na 'asisti' mbili, na klabu anayohusishwa nayo ya Azam, ndio imemvuruga na kuona haitaji tena kubakia Yanga.

Mkataba wa Yanga na Fei Toto kwa sasa umebakiza mwaka mmoja na nusu na klabu yake iko tayari kukaa naye meza moja ili kuboresha mshahara aliokuwa anaupata wa Sh milioni nne hadi kufikia Sh. milioni 10.

Inadaiwa akisaini Azam atapokea kitita cha Sh. milioni 390, mshahara wa Sh. milioni 17 kila mwezi, gari ya thamani, nyumba ya kuishi yenye thamani ya Sh. milioni 10 kwa mwezi pamoja na vitu vingine mbalimbali.

Wakati huo huo, kikosi cha Yanga juzi kilimtembelea mlezi wa timu hiyo, Mama Fatma Karume, kabla ya kurejea Dar es Salaam baada ya kuondolewa katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi yanayoendelea Visiwani, Zanzibar.

Yanga sasa itarejea kwenye uwanja wa mazoezi ili kufanya maandalizi ya mechi zake tatu za Ligi Kuu Tanzania Bara zinazofuata dhidi ya Ihefu SC, Ruvu Shooting na Namungo na baadaye kushuka dimbani kuendelea kutetea taji lake la michuano ya Kombe la FA.

## Robertinho aanza kuwasoma Yanga

INATOKA UK. 24

ili kuniwezesha kuwajua wachezaji na kuwapa mbinu zangu, nitahakikisha tunafikia malengo yanayotarajiwa," alisema kocha huyo.

Aliongeza wakiwa Dubai wanatarajia kucheza michezo miwili ya kirafiki ambayo itawaweka imara kabla ya kurejea nchini Januari 14, mwaka huu na siku tatu baadaye itawakaribisha Mbeya City kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa. Wakati huo huo, Simba inatajwa iko katika hatua za mwisho za mazungumzo na straika, raia wa Zambia, Kennedy Musonda (29), ambaye anatokea Power Dynamos ili kusaidiana na Moses Phiri kwenye nafasi ya ushambuliaji.

Ingawa hakumtaja jina, Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alithibitisha klabu yake ipo katika hatua za mwisho za kuvunja mikataba ya wachezaji, ambao ni straika na kiungo mkabaji ili kukiongezea nguvu kikosi chao.

"Simba tuko katika mchakato wa kuzungumza na wachezaji tunaowakusudia, wapo ambao tunazungumza nao kwa sababu kwenye eneo la ushambuliaji bado hatujaridhika, kama vile haitoshi tunaangalia pia katika eneo la ukabaji tunatafuta watu, kila kitu kikiwa tayari tutawajulisha, cha muhimu ni wanachama na mashabiki wa Simba wakae kwa kutulia," alisema Ahmed. Vyanzo vya habari kutoka nchini Zambia vinasema klabu hizo mbili zimekubaliana baada ya mazungumzo ya muda mrefu ambapo Simba imelazimika kuvunja mkataba kwa kulipa zaidi ya Sh. milioni 350 ili kufanikisha usajili huo.

Musonda anatajwa kuwa chaguo la pili baada ya Cesar Manzoki anayekipiga Dalian FC ya China kukosekana, lakini habari kutoka Uganda zinadai mchezaji huyo kwa sasa ni majeruhi, hivyo Simba isingewezekana kumsajili.

Musonda ambaye pia alikuwa akiwaniwa na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), amepachika mabao 11 kati ya mechi 17 ambazo ameichezea Power Dynamos inayoongoza katika Ligi Kuu Zambia wakiwa na pointi 35.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAPILI - 08/01/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 4908 | Fatih Karagumruk vs Konyaspor | 2.69 | 3.38 | 2.46 |
| 14:00 | 3437 | Covilha vs Vilafranquense | 3.15 | 3.15 | 2.22 |
| 14:00 | 4019 | Gokulam Kerala FC vs Churchill Brothers | 2.34 | 3.15 | 2.81 |
| 14:15 | 5013 | Utrecht vs Feyenoord | 3.76 | 3.81 | 1.81 |
| 14:30 | 5803 | Salernitana vs Torino | 3.53 | 3.13 | 2.10 |
| 15:00 | 1828 | Posta Rangers vs Gor Mahia | 3.60 | 2.77 | 2.17 |
| 15:00 | 4823 | AFC Leopards vs Bidco United | 2.09 | 2.91 | 3.59 |
| 15:30 | 1614 | Bristol City vs Swansea | 2.85 | 3.20 | 2.37 |
| 15:30 | 2226 | Racing Genk vs Brugge | 2.13 | 3.62 | 3.03 |
| 15:30 | 2560 | Derby vs Barnsley | 1.99 | 3.40 | 3.45 |
| 15:45 | 5798 | Haras EL Hodood vs Ismaily SC | 3.88 | 2.89 | 2.12 |
| 16:00 | 3265 | Almeria vs Real Sociedad | 3.85 | 3.35 | 1.95 |
| 16:30 | 1607 | Motherwell vs Hibernian | 2.83 | 3.22 | 2.43 |
| 16:30 | 3119 | Cambuur vs FC Volendam | 1.90 | 3.66 | 3.56 |
| 16:30 | 5144 | NEC Nijmegen vs Ajax | 6.94 | 5.15 | 1.35 |
| 17:00 | 1461 | Spezia vs Lecce | 2.57 | 3.02 | 2.77 |
| 17:00 | 1806 | Hartlepool vs Stoke City | 5.52 | 4.14 | 1.51 |
| 17:00 | 2690 | Stockport vs Walsall | 1.75 | 3.55 | 4.34 |
| 17:00 | 3346 | Cardiff vs Leeds | 3.86 | 3.66 | 1.81 |
| 17:00 | 3916 | Hamrun Spartans vs Hibernians | 1.94 | 3.22 | 3.66 |
| 17:00 | 4109 | Norwich City vs Blackburn | 1.82 | 3.60 | 3.90 |
| 17:00 | 5141 | Lazio vs Empoli | 1.52 | 4.16 | 5.55 |
| 17:00 | 5352 | Volos vs Olympiakos | 8.95 | 4.58 | 1.34 |
| 18:00 | 1025 | Atromitos vs Ionikos Nikea FC | 1.81 | 3.28 | 4.58 |
| 18:00 | 2288 | Zulte Waregem vs Mechelen | 2.78 | 3.68 | 2.26 |
| 18:00 | 4259 | Pafos FC vs Apollon Limassol | 2.09 | 3.36 | 3.41 |
| 18:15 | 3525 | Rayo Vallecano vs Betis | 2.33 | 3.19 | 3.04 |
| 18:30 | 4307 | TS Galaxy FC vs Stellenbosch | 2.16 | 2.82 | 3.80 |
| 18:30 | 4397 | Mtarfa FC vs Mqabba FC | 2.85 | 3.55 | 2.28 |
| 18:30 | 5203 | Pacos Ferreira vs GD Chaves | 2.79 | 3.18 | 2.49 |
| 18:45 | 2726 | SBV Excelsior vs Groningen | 2.61 | 3.50 | 2.43 |
| 19:00 | 1366 | Fenerbahce vs Galatasaray | 2.09 | 3.48 | 3.23 |
| 19:00 | 5441 | Dundee Utd vs Rangers | 8.18 | 5.18 | 1.32 |
| 19:30 | 2420 | Manchester City vs Chelsea | 1.40 | 4.51 | 6.81 |
| 19:30 | 3774 | Aston Villa vs Stevenage | 1.14 | 7.08 | 14.76 |
| 20:00 | 1517 | Talaea El Gaish vs Arab Contractors | 2.57 | 2.77 | 3.07 |
| 20:00 | 1546 | Aris Salonica vs Asteras Tripolis | 1.57 | 3.78 | 5.76 |
| 20:00 | 1633 | Dunkerque vs AJ Auxerre | 4.09 | 3.59 | 1.81 |
| 20:00 | 1644 | Sampdoria vs Napoli | 7.52 | 4.65 | 1.37 |
| 20:00 | 1698 | Lannion FC vs Toulouse | 13.98 | 6.79 | 1.17 |
| 20:00 | 4820 | AEL Limassol vs Apoel Nicosia | 4.02 | 3.46 | 1.88 |
| 20:30 | 1925 | Anderlecht vs Union Saint Gilloise | 2.65 | 3.35 | 2.50 |
| 20:30 | 4055 | AEK Athens vs Panathinaikos | 1.84 | 3.24 | 4.48 |
| 20:30 | 5312 | Sevilla FC vs Getafe | 1.75 | 3.36 | 5.01 |
| 21:00 | 4425 | Maritimo vs Sporting Lisbon | 7.56 | 4.67 | 1.37 |
| 22:45 | 1905 | Lille vs Troyes | 1.42 | 4.57 | 6.56 |
| 22:45 | 5149 | AC Milan vs Roma | 1.83 | 3.42 | 4.17 |
| 23:00 | 2052 | OH Leuven vs Kortrijk | 1.68 | 3.99 | 4.39 |
| 23:00 | 3739 | Atletico Madrid vs Barcelona | 2.93 | 3.22 | 2.39 |
| 23:30 | 5885 | Boavista vs Gil Vicente | 2.59 | 3.23 | 2.64 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Januari 8, 2023

Nipashe





**Ten Hag afunguka Rashford hazuiliki** UKURASA 21




Mlezi wa Yanga, Mama Fatma Karume (katikati), akiwa na Rais wa klabu hiyo, Hersi Said (kushoto), makamu wake, Arafat Haji pamoja na wachezaji wa timu hiyo walipoenda kumtembelea nyumbani kwake eneo la Maisara jana asubuhi. Yanga imetolewa katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi na tayari imerejea jijini, Dar es Salaam. **PICHA: SAADA AKIDA**

# SAA ZAHESABIKA HATIMA FEI TOTO

## Jangwani yasema haendi kokote huku ikifuata ubani kwa Mama Karume kwa...

**Na Saada Akida**

WAKATI Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), ikisema kiungo, Feisal Salum maarufu Fei Toto ni mchezaji wa Yanga, hatima ya shauri lililowasilishwa na klabu hiyo ya mitaa ya Jangwani na Twiga, Kariakoo, Dar es Salaam itajulikana rasmi kesho, imeelezwa.

Yanga iliwasilisha malalamiko yake TFF baada ya Fei Toto kutangaza kuvunja mkataba na klabu hiyo na kulipa kiasi cha Sh. milioni 112 kutokana na uamuzi huo aliofikia, fedha ambazo mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara walizirudisha kwenye akaunti ya mchezaji huyo.

Ofisa Habari wa TFF, Clifford Ndimbo, alisema jana katika taarifa yake kamati imeamua Fei Toto bado ni mchezaji wa Yanga kwa mujibu wa mkataba.

Ndimbo alisema hatima kamili ya sakata hilo itajulikana kesho baada ya uamuzi kamili kwa pande zote mbili kati ya nyota huyo na klabu yake kukamilisha maelezo.

"Uamuzi kamili kwa upande zote mbili zilizokuwa zinahusika katika shauri hilo utatolewa Jumatatu, Klabu ya Yanga iliwasilisha malalamiko mbele ya kamati hiyo ikipinga hatua ya mchezaji wao kuvunja mkataba kati yao bila ya kuwashirikisha," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Ilisema Kamati ya Sheria na Hadhi za wachezaji iliyokutana jijini juzi ilisikiliza malalamiko hayo ambapo pande zote mbili ziliwakilishwa na wanasheria na kufanyia kazi na kesho itatoa hukumu kamili kuhusiana na shauri hilo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Rais wa Yanga, Hersi Said, alisema wanatambua kiungo huyo bado ni mchezaji wao halali na watasubiri uamuzi utakaotolewa na mamlaka husika.

"Kwa sasa akili na nguvu zetu tunazielekeza katika michezo iliyopo mbele yetu, ikiwamo ya ligi na michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika," alisema Hersi.

Kwa sasa Fei Toto hayuko katika kambi ya Yanga na alionekana amekwenda Dubai katika mapumziko mafupi kabla ya kurejea nchini ili kusikiliza wito kutoka TFF.

Kabla ya kusafiri, Mzanzibari huyo aliandika waraka wa kuwaaga na kuwashukuru mashabiki, wanachama na viongozi wa Yan-

INAENDELEA UK. 23

## Robertinho aanza kuwasoma Yanga

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

KOCHA mpya wa Simba, Roberto Oliveira 'Robertinho', ameanza na mambo matatu ndani ya timu hiyo ikiwamo kukiona kikosi kamili, kufanya tathimini ya Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na kufuatilia 'mafaili' ya wapinzani wao katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika Simba iko Kundi C na timu za Raja Casablanca ya Morocco, Horoya AC (Guinea) na Vipers ya Uganda, timu ya zamani ya Robertinho.

Licha ya Robertinho kuwafahamu nje, ndani, Vipers ya Uganda ameamua kuwaweka kiporo na kuanza kuwapeleleza Horoya AC ambao watacheza nao mechi ya kwanza katika hatua ya makundi ya michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Ili kujiweka imara, kikosi cha Simba kikiwa na msafara wa watu 38 kiliondoka nchini jana na kuelekea Dubai, Falme za Kiarabu ili kuweka kambi ya mazoezi ya siku saba kujiandaa na mechi za Ligi Kuu na mashindano mengine wanayoshiriki.

Kambi hiyo ni mwaliko kutoka kwa Rais wa heshima wa klabu ya Simba, Mohammed Dewji 'Mo Dewji' ili kuipa timu nafasi nzuri ya kujiimarisha na hatimaye kutimiza malengo yake.

Akizungumzia kambi hiyo, Robertinho alisema ni uamuzi sahihi uliofanya na mabosi wake na anaamini utampa nafasi ya kuangalia kikosi chake kwa mapana.

Kocha huyo alisema ataanza kupandikiza falsafa zake akishirikiana na makocha wasaidizi, Juma Mgunda na Selemani Matola, kwa ajili ya kuboresha kiwango cha timu hiyo iliyoko katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Ni uamuzi mzuri kwa uongozi kunipa muda wa kufanya mazoezi na kikosi kwa utulivu

INAENDELEA UK. 23


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >